

# Mawazo Juu ya Maisha ya Roho



Taasisi ya Ruhi





Kitabu cha 1

# Mawazo Juu ya
# Maisha ya Roho

Taasisi ya Ruhi

Vitabu katika mlolongo:

Hapa chini yapo majina ya vitabu katika mlolongo ulioandaliwa na Taasisi ya Ruhi. Vitabu hivi vinakusudiwa kutumika kama mlolongo mkuu wa kozi katika juhudi ya hatua kwa hatua ya kuongeza uwezo wa vijana na watu wazima kutumikia jumuiya yao. Taasisi ya Ruhi pia ina kuza kundi moja la kozi zinazochepuka kutoka kitabu cha tatu katika mlolongo kwa ajili ya kuwafunza Waalimu wa madarasa Bahá'í ya watoto, na hili limeelezwa katika orodha vile vile. Lazima ionwe kuwa orodha itapitia mabadiliko kadri uzoefu katika uwanja huu yanavyoendelea, na majina mapya yataongezwa kadri idadi inayoongezeka ya vipengele vya kimtaala vinavyoendelea kukuzwa ili vikifikie hatua hii ambapo vinaweza kusambazwa kwa upana.

| | |
|---|---|
| Kitabu cha 1 | *Mawazo Juu ya Maisha ya Roho* |
| Kitabu cha 2 | *Uinukaji kwa Kuhudumu* |
| Kitabu cha 3 | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 1* |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 2* (kozi ya mchepuo) |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 3* (kozi ya mchepuo) |
| | *Kufundisha Madarasa ya Watoto, Daraja la 4* (kozi ya mchepuo) |
| Kitabu cha 4 | *Wadhihirishaji Pacha* |
| Kitabu cha 5 | *Ufungukaji wa Uwezo wa Vijana Chipukizi* |
| | *Msukumo wa Awali: Mchepuo wa kwanza wa kozi ya Kitabu cha 5* |
| | *Kupanua Duara: Mchepuo wa pili wa kozi ya Kitabu cha 5* |
| Kitabu cha 6 | *Ufundishaji wa Hoja* |
| Kitabu cha 7 | *Kutembea Pamoja katika Njia ya Huduma* |
| Kitabu cha 8 | *Ahadi ya Bahá'u'lláh* |
| Kitabu cha 9 | *Kupata Mtazamo wa Kihistoria* |
| Kitabu cha 10 | *Kujenga Jumuiya Hai na Zenye Kupuma* |
| Kitabu cha 11 | *Nyenzo za Kimwili* |
| Kitabu cha 12 | *Familia na Jumuiya* |
| Kitabu cha 13 | *Kujihusisha katika Shughuli za Kijamii* |
| Kitabu cha 14 | *Kushiriki katika Mijadala ya Umma* |

Haki miliki © 1999, 2013, 2020 na Ruhi Msingi, Colombia
Haki zote zimehifadhiwa. 4.1.3.PE Zilizochapishwa Machi 2021
ISBN 978-958-52941-8-9

Kilichapishwa awali kwa Kihispania kama *Reflexiones sobre la vida del espíritu*
Haki miliki © 1987, 1995, 2008, 2020 na Ruhi Msingi, Colombia
ISBN 978-958-59880-3-3

Taasisi ya Ruhi
Cali, Colombia
Barua pepe: instituto@ruhi.org
Tovuti: www.ruhi.org

# Yaliyomo

Mawazo Machache kwa ajili ya mkufunzi .................... v

Ufahamu wa Maandiko ya Kibahá'í .............................. 1

Sala.................................................................... 13

Uhai na Kifo................................................................ 29

# Mawazo Machache kwa ajili ya Mkufunzi

Idadi ya maeneo ambamo *Mawazo Juu ya Maisha ya Roho*, kitabu cha kwanza cha mlolongo mkuu wa kozi zilizotolewa na Taasisi ya Ruhi, kinasomwa kila mahali ulimwenguni inaendelea kukua katika kipindi cha miaka mingi. Katika hali nyingi, zana husomwa na kujadiliwa na kikundi cha marafiki, ambao pengine ni kikundi cha mafunzo kinachokutana kila mara, kinaweza kukutana katika kampeni iliyoandaliwa kwa ajili ya masomo kabambe, au wanaweza kukusanyika katika kambi wakati wa likizo za shule. Lolote liwalo tukio, mjumbe mmoja wa kikundi atakuwa mkufunzi. Uhusiano kati ya mkufunzi na washiriki wengine siyo ule unaofanana na wa mwalimu na mwanafunzi; wote wanahusika kwa utambuzi kamili katika mchakato ambamo kila mmoja anajitahidi kujifunza. Lakini mkufunzi siyo mrahisishaji anayejitenga na asiyesema kitu aidha wakati wa majadiliano. Akiwa amemaliza kusoma idadi ya kutosha ya kozi zilizomo katika mlolongo na kufanya vitendo vya huduma, wanavyotiwa moyo, anaweza kumsaidia kila mjumbe wa kikundi kufanikisha kupata kusudi la zana wanazosoma. Itawasaidia wale ambao wanafanya kazi ya ukufunzi wa Kitabu cha 1 kupitia mawazo yaliyowasilishwa katika utangulizi huu mara kwa mara.

Washiriki duniani kote huja kwenye kozi hii ya kwanza ya taasisi kutoka usuli tofauti. Baadhi tayari ni wajumbe wa jumuiya ya Kibahá'í ambao wanategemea kuongeza uwezo wao wa kuihudumia Hoja ambayo wao wameikumbatia. Wengine wanaiona kozi hii kama mwanzo wa uchunguzi wao wa Imani ya Kibahá'í kama dini. Bado wengine wanavutiwa kwa mawazo ya Kibahá'í na wangependa kujifahamisha wenyewe malengo na jitihada za jumuiya. Na ipo haswa idadi inayozidi kuongezeka ya vijana ambao wangependa kukuza uwezo wao wa kuitumikia jamii, aghalabu kupitia programu moja au nyingine inayoendelezwa na jumuiya ya Kibahá'í, wao huchukua kozi kama hatua ya mwanzo.

Tangu mwanzoni inabidi iwe wazi kwa kila mshiriki kuwa kozi za Taasisi ya Ruhi zinachora njia ya huduma kwa jamii ya wanadamu, ambayo juu yake kila mmoja wetu anatembea kwa mwendo wake, akisaidia na akisaidiwa na wengine. Kukanyaga juu ya njia hii inamaanisha ufuatiliaji wa kusudi la kimaadili lenye pande mbili: kufuatilia ukuaji wa kiroho na kiakili wa mtu binafsi, na kuchangia kwa mabadiliko ya jamii. Maendeleo juu ya njia hii yanamaanisha ukuzaji wa idadi fulani ya uwezo ambao unahitaji uelewa na ujuzi, sifa za kiroho na mielekeo inayostahili sifa, hali kadhalika na safu ya uwezo na ujuzi. Vyanzo vya maarifa ambavyo kutoka kwavyo vitabu vya Taasisi huchota kwa upande mmoja, mafundisho ya Imani ya Kibahá'í na, kwa upande mwingine, tajiriba inayoendelea kukusanyika ya jumuiya ya Kibahá'í ulimwenguni katika kuendeleza ustaarabu wa kimwili na wa kiroho. Ni maono ya Bahá'u'lláh ya jinsi mtu binafsi anavyoweza kuwa na ustaarabu tunaoweza kuujenga unaoitia msukumo Taasisi. Inadhaniwa kuwa washiriki wote, bila kujali usuli wao wako wazi kuukumbatia muono huu, ambao ni dhahiri katika kila kitengo cha kila kitabu.

Katika ulimwengu ambamo itikadi na falsafa viko tayari kutumia kila njia inayowezekana kwa ajili ya kupata wafuasi, mtu ambaye haijui vizuri Imani pengine anaweza kuwa na maswali halisi juu ya madhumuni ya Taasisi ya Ruhi, hususan, "Je, ninaambiwa kubadili dini yangu?" au "Je, ninaombwa kujiunga na dini fulani?" Maswali kama hayo yanampa mkufunzi nafasi ya kueleza kusudi la mlolongo wa kozi kama ilivyoelezwa hapo

juu. Ambapo ni kawaida kuwa Wabahá'í wangekuwa wenye shauku kuwaona marafiki zao wakijiunga na jumuiya, mafundisho yao wenyewe yanawazuia, kutoka kujaribu kuwageuza dini, pengine mkufunzi angependa kuongeza kusema. Kutembea Njia ya Huduma iliyofunguliwa na kozi za taasisi huitisha uelewa unaoendelea kukua wa Mafundisho ya Bahá'u'lláh, ambayo zana zinajitahidi kuweka wazi bila mashaka; kukubali na imani ni masuala yanayohitaji kufikiriwa na kila mtu binafsi kwa uhuru na bila shinikizo.

Siyo jambo la kushangaza hivyo, ni kwenye swali la uelewa, ambalo ni kiini katika vitabu vyote vya mlolongo, kwamba hili huanza. Kusoma kutoka Maandiko Matakatifu siyo sawa na kusoma maelfu ya kurasa ambazo mtu huziona maishani mwake, na kitengo, "Ufahamu wa Maandiko ya Kibahá'í", hutafuta kulea desturi ya kusoma vifungu kutoka Vitabu Vitakatifu kila siku na kutafakari juu ya maana yao, desturi ambayo itawasaidia sana washiriki kadri wanavyoanza safari yao juu ya njia ya huduma. Kuwaongoza katika masomo yao, mkufunzi afikirie sana juu ya suala la uelewa.

Maandiko ya Kibahá'í yana kweli za kiroho zenye kina, na wakati tunajaribu kwenda mbele katika uelewa wa maana yao yasio na mwisho, tunajua hatuwezi asilani kufika mwisho kabisa. Kwa kawaida tunapata uelewa wa msingi wa maana ya papo hapo ya kifungu kimoja tunapokisoma kwa mara ya kwanza, na Sehemu ya 1 ya kitengo hiki hupachukulia hapo kama mahali pa kuanzia. Kwa hiyo, baada ya kusoma dondoo hii, "Uboreshaji wa ulimwengu unaweza kutimizwa kwa matendo safi na mema, kwa mwenendo usifikao na unaostahili", washiriki wanaulizwa tu, "Uboreshaji wa ulimwengu unaweza kutimizwaje?" Kwa mtazamo wa haraka, sehemu kubwa ya maswali na mazoezi ya aina hii yanaonekana kuwa rahisi sana. Lakini miaka mingi ya tajiriba inaonekana kuthibitisha uamuzi wa Taasisi wa kuanza kwa namna hii. Sote tunahitaji kukumbushwa kuwa, katika haraka yake ya kutafuta tabaka za ukweli katika fungu moja, akili haipaswi kupuuzia maana yake dhahiri. Umakini kwa ngazi hii ya kwanza ya uelewa pia unadhihirika kuwa muhimu kwa ushauriano wa kikundi; huongeza nguvu za wazo la umoja, ambao hupatikana kwa urahisi pale ambapo maoni ya mtu binafsi yanakubali kuangazwa kwa hekima Takatifu.

Ni muhimu hapa kuona kuwa uelewa wa maana ya sehemu kubwa ya vifungu haupati faida kwa maongezi marefu juu ya neno moja moja nje ya muktadha mzima. Baada ya kusema hayo, wakati mwingine, pengine itabidi kuangalia neno katika kamusi. Kile ambacho kingefaa zaidi, hata hivyo, ni kwamba washiriki watajifunza jinsi ya kuelewa maana ya maneno kutoka sentensi na aya.

Ili uelewa uweze kupanuka mbele zaidi ya ufalme wa maana yake ya papo hapo, mifano inayoonesha jinsi mawazo yanavyoweza kuelezwa inaweza kusaidia. Kile kinachohitajika ni kuhusu suala hili ni mazoezi yaliyo wazi. Katika Sehemu ya 2, kwa mfano, washiriki wanaombwa kuamua, kufuatana na kifungu walichosoma hivi punde, kama baadhi ya tabia ni stahiki. Katika zoezi kama hilo katika Sehemu ya 4, wanahamasishwa kutaja sifa njema tano na halafu kuamua kama inawezekana kupata hata moja kati yao bila ukweli — kama ilivyoelezwa katika Maandiko kuwa ni "msingi wa njema zote za binadamu".

Ili kufanikisha kusudi lake, kitengo hiki kinadai maendeleo zaidi katika uelewa kwa kuwapa washiriki changamoto, kufikiria juu ya baadhi ya matokeo ya vifungu vilivyowasilishwa. Katika Sehemu ya 2, wanatakiwa kuamua kama tamko hili "Watu wema duniani ni wachache mno kwamba matendo yao hayana matokeo yoyote" ni ukweli. Hapa kusudi siyo la kupata maoni zaidi. Mkufunzi lazima asite kidogo na kuhoji sababu kwa ajili ya majibu ya washiriki. Kwamba tamko hilo lazima siyo kweli kwa sababu linapinga nukuu ya kwanza iliyomo katika sehemu iliyotangulia ni hatma ambayo kikundi sharti kifikiriye.

Swali kwamba kama Wabahá'í wanaweza kuungama dhambi yao kwa wengine pia ni mfano wa aina hii ya zoezi. Linaongelea makatazo yaliyomo katika mafundisho dhidi ya kuungama kama njia ya kusamehe dhambi, kitu ambacho ingawa hakikutajwa mahususi katika vifungu vyovyote vilivyosomwa, kinaweza kueleweka kwa kuchunguza maana ya aya hii, "Jifanyie hesabu mwenyewe kila siku kabla hujaitwa kwenye kutoa hesabu".

Kwa vyovyote mazoezi katika kitengo hiki hayajaribu kuzingira maana nyingi mbalimbali zilizomo katika vifungu vinayoongelewa. Swali moja ambalo kila mkufunzi lazima alifikirie ni muda ambao unapaswa kutumika kuongelea zoezi lolote lile. Hapa ni muhimu kuweka akilini kuwa urefushaji wa maongezi kwa kutambulisha mawazo mengi yanayohusika lakini ni ya pembeni hupunguza ufanisi wa zana. Kila kikundi huhitaji kuanzisha mdundo unaoridhisha wa maendeleo, washiriki sharti wahisi kwamba wao wanasogea kwa uthabiti kufuatana na uwezekano wao wenyewe. Mkufunzi, hata hivyo, lazima awe makini, isitokee kuwa sehemu zinapitiwa kwa haraka na kijuujuu bila upembuzi wenye fikra wa mazoezi; vikundi vilivyoendelea kwa njia hii, kwa kujaza majibu tu, kamwe havitapata matokeo ya kudumu.

Kipengele kimoja cha mwisho kinastahili kutajwa hapa: ni juu ya mkufunzi kuhakikisha kuwa kila mjumbe wa kikundi anaendelea kushughulika katika mchakato wa kujifunza unaoendelezwa na zana hizi. Kukaribisha ushirikiano bila kumlazimisha mtu yeyote kuongea aghalabu ni changamoto. Kile ambacho kinapaswa kutambuliwa kutoka mwanzo ni kwamba changamoto hii kwa nadra inatimizwa kwa kuuliza maswali kama vile, "Hii ina maana gani kwako?" Maswali ya aina hii yanaupunguza ufahamu na ukweli kwenye kiwango ya maoni. Na hapo inakuwa vigumu kujenga mandhari ambamo ushauriano miongoni mwa wajumbe wa kikundi haswa wanaweza kupata uelewa uliyoongezeka.

Kitengo cha pili katika kitabu hiki kinahusu, kama kile cha kwanza desturi muhimu kwa maisha ya kiroho: kusali mara kwa mara. Kinaweka katika sehemu ya ufunguzi wazo la "njia ya huduma", na kupendekeza kuwa, ili kutembea njia hii, lazima tuwe tumejaa madhumuni ya pande mbili. Washiriki wachunguze seti za mwanzoni za mateuzi zinazotoa umaizi katika asili ya kusudi hili, mada ambayo itaongelewa zaidi katika kozi za siku za mbele.

Pamoja na mazingira ya mada hii kitengo hiki huanza uchunguzi wake juu ya maana ya sala. Kinachukua njia inayofanana na ile iliyoelezwa katika vifungu vilivyotangulia. Maswali na mazoezi yanaundwa ili yaweze kusogeza mbele uelewa wa maana ya vifungu kutoka katika Maandiko ambayo yanasomwa. Kadri kikundi kinavyoendelea kupitia kitengo hiki, mkufunzi pengine atahitaji kuondoa mashaka kwa kuchambua mawazo yaliyojikita katika ufafanuzi na mazoea ya siku zilizopita. Katika tamaduni fulani, mila na mwonekano polepole vimefunika umuhimu wa hali ya ndani, na wengi hupuuzia hitaji la kusali, kitu ambacho, kwa roho ya binadamu, hakipungui katika umuhimu kuliko chakula cha kulisha mwili.

Juu ya yote, kwa hiyo, kitengo hiki kinatarajia kuamsha ndani ya washiriki shauku ya "kuongea na Mungu" na kusogea karibu Yake. Miongoni mwa mawazo yaliyoongelewa lipo wazo juu ya maana ya kuingia katika hali ya ibada, mwelekeo wa mioyo na akili, tufanyapo hivyo, na hali zinazopaswa kujengwa katika mazingira yetu, ama tukiwa peke yetu, au katika mkusanyiko. Kwa uhakika, baada ya kufikiria kidogo juu ya nguvu zinazozalishwa kupitia ibada ya pamoja, washiriki wanaombwa kufikiria kukaribisha mkusanyiko kwa ajili ya kusali pamoja na ibada.

Usomaji wa kitengo cha tatu cha kitabu, "Uhai na Kifo", kinatarajiwa kitaimarisha azma ya Kutembea Njia ya Huduma na kuijalia maana ya ndani zaidi. Huduma katika

ulimwengu huu inaeleweka vizuri zaidi katika muktadha kamili wa maisha, ambayo huenda mbele zaidi ya uwepo wetu wa ulimwenguni na huendelea daima kadri roho zetu zinavyo endelea kila mahali kupitia malimwengu ya Mungu. Katika mchakato wa elimu, kinyume na mafunzo ya kiufundi, washiriki wanapaswa kuwa watambuzi zaidi kuhusu maana na umuhimu wa kile wanachokifanya. Ni pale tu kama utambuzi huo hukua, tajiriba huonesha, ndipo watakapoweza kujiona imara, "wamiliki" wa ujifanzaji wao wenyewe.

Kila sehemu ya kitengo hiki hufunguka kwa dondoo moja hadi tatu kutoka Maandiko Kibahá'í, ikifuatwa na mazoezi machache. Lugha ya vifungu vilivyonukuliwa katika kitengo hiki ni ngumu zaidi kuliko vile viwili vilivyotangulia. Hakuna haja bila shaka, kwa kikundi kutumia muda mrefu juu ya maneno magumu; mkufunzi atataka kuhakikisha kuwa kila mmoja anatambua wazo kuu linaloongelewa katika kila sehemu, kitu maalum ambacho mazoezi yanajaribu kukitekeleza.

Kutokana na asili ya somo, mazoezi yanayohusu mifano halisi ni machache na mbali kati yao. Sehemu kubwa inafanya kazi kwenye ngazi ya kinadharia. Kile kinachohitaji kuangaliwa ni kwamba baadhi ya maswali yanayoulizwa katika mazoezi hayawezi kujibiwa kwa haraka, au kwa urahisi. Yanatambulishwa kwa ajili ya kuinua utambuzi kuhusu somo; kama washiriki wakifikiria maswali kama haya tu, lengo la ujifunzaji litakuwa limetimizwa.

Sehemu kadhaa za mwanzo zinalenga juu ya uhusiano kati ya roho na mwili, ambavyo kwa pamoja, vinamfanya mwanadamu katika ulimwengu huu wa uwepo. Wazo kuu linalowasilishwa katika sehemu hizi ni kwamba roho siyo kitu cha kimwili; ushirikiano wake na mwili unaweza kufananishwa na mwangaza unaoonekana katika kioo. Wala vumbi lifunikalo ubapa wa kioo ama hata uvunjikaji wa kioo unaoweza kutokea mwishowe vinaweza kuathiri uzuri wa mwangaza wenyewe. Kifo ni badiliko tu la hali, pale ushirikiano kati ya mwili na roho unapovunjika; baadaye, roho huendelea milele kuelekea kwa Muumba wake.

Kitengo hiki hugeukia baadaye kwenye swali la kusudi la maisha—kumjua Mungu na kufika Mbele Yake. Majadiliano hapa yanazungukia dhima mbili pana. Ya kwanza ni kusudi la maisha yetu katika ulimwengu huu na ya pili ni safari ya roho baada ya kifo. Roho ni alama ya Mungu na inaweza kuakisi majina Yake yote na sifa. Hata hivyo uwezo uliyomo ndani ya mwanadamu umejificha, unaweza kukuzwa tu kwa msaada wa Wadhihirishaji wa Mungu, Viumbe wale waliotakasika Ambao huja wakati baada ya wakati kwa ajili ya kuongoza wanadamu. Kupitia elimu ya kiroho Wao wanayoleta, hazina zilizofichwa zinaweza kufunuliwa.

Kuhusu safari ya roho baada ya kifo, mfululizo wa mawazo umewekwa wazi kwa ajili ya washiriki kufikiria: kwamba wale waaminifu kwa Mungu watapata furaha ya kweli; kwa kuwa hakuna yeyote kati yetu anayeweza kujua mwisho wetu wenyewe, na kwa hiyo inatubidi kila mmoja wetu tusameheane, na tusjihisi bora kwa wengine; kwamba katika ulimwengu ujao, kama katika ulimwengu huu, roho itaendelea katika maendeleo yake na vipawa vya kiroho tulivyokuza hapa vitakuwa vyenye msaada na vitatusaidia huko, kwamba tutawatambua wapendwa wetu katika falme za mbele zaidi, watakumbuka maisha yetu katika ulimwengu huu, na watafurahia urafiki na roho takatifu na zilizotakasika.

Kitengo kinafikia tamati na kifungu kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh ambamo tunahakikishiwa manufaa ya ulimwengu ujao na kuhimizwa kuwa tusiruhusu mabadiliko na fursa za ulimwengu huu kutuletea huzuni. Washiriki wanaombwa kutafakari, halafu, juu ya matokeo ya yote waliyoyasoma kwa ajili ya maisha yao wenyewe.



# Ufahamu wa Maandiko ya Kibahá’í

Kusudi

Kukuza tabia ya kusoma nukuu kutoka
Maandiko Matakatifu kila siku na
kutafakari juu ya maana zake

## SEHEMU YA 1

Kusudi la kitengo hiki ni kukusaidia kukuza na kuongeza nguvu za tabia ya kusoma vifungu kutoka Maandiko Matakatifu kila siku na kutafakari juu ya maana yao. Kitengo hiki kinaanza kwa zoezi rahisi ambalo linakuambia kusoma tamko la sentensi moja kutoka Maandiko na kujibu swali moja, jibu ambalo ni tamko lenyewe. Ingawa ni rahisi kufanya, zoezi litakusaidia kutafakari juu ya maana ya matamko yaliyonukuliwa na kuyakariri.

**"Uboreshaji wa ulimwengu unaweza kutimizwa kwa matendo safi na mema, kwa mwenendo usifikao na unaostahili."[1]**

1. Uboreshaji wa ulimwengu unaweza kutimizwaje? ____________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**"Jihadharini, Enyi watu wa Bahá, msije mkatembea katika njia za wale ambao maneno yao hutofautiana na matendo yao."[2]**

2. Je, katika njia za watu gani tusitembee?______________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**"Ewe Mwana wa Kuwa! Jifanyie hesabu mwenyewe kila siku kabla hujaitwa kwenye kutoa hesabu . . ."[3]**

3. Je, yatupasa kufanya nini kabla hatujaitwa kutoa hesabu?_______________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

**"Sema: Enyi ndugu! Acha vitendo, siyo maneno, viwe pambo lenu."[4]**

4. Pambo letu la. kweli lafaa kuwa nini? ______________________________________

______________________________________________________________________

**"Maneno matakatifu na matendo safi na mema hupaa hadi mbingu ya utukufu wa mbinguni."[5]**

5. Maneno matakatifu na matendo safi na mema hufanya nini? ____________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 2

Hapa chini yapo maswali kadhaa yanayohusu mateuzi ambayo mmekwisha yasoma. Yamekusudiwa kukusaidia kutafakari zaidi juu ya maana ya vifungu katika kikundi chako na haipaswi kufanywa bila kufikiri. Hii haina maana ya kusema kuwa kila zoezi linahitaji kuongelewa kwa muda mrefu. Kama swali lina changamoto, hata hivyo, mkufunzi wa kikundi chako atakusaidia kulichunguza kikamilifu.

1. “Kisifikacho” humaanisha kitu kistahilicho sifa. Ni yapi kati ya yafuatayo yanastahili sifa?

   _____ Kuwa mfanyakazi mzuri

   _____ Kuheshimu wengine

   _____ Kuwa mwenye bidii katika masomo

   _____ Kuwa muongo

   _____ Kuwa mvivu

   _____ Kuhudumia wengine

2. Nini maana ya fungu la maneno “kabla hujaitwa kwenye kutoa hesabu”? __________

   ________________________________________________________________________

3. Ni zipi kati ya kauli zifuatazo ni kweli?

   _____ Watu wema duniani ni wachache mno kwambamatendo yao hayana matokeo yoyote.

   _____ Jambo fulani ni sahihi likikubaliana na maoni ya watu wengine.

   _____ Jambo fulani ni sahihi likikubaliana na Mafundisho ya Mungu.

4. Ni yapi ya yafuatayo ni matendo safi na mema?

   _____ Kutunza na kufundisha watoto

   _____ Kuiba

   _____ Kuomba kwa ajili ya maendeleo ya wengine

   _____ Kusema uongo mdogo ili kuepuka taabu

   _____ Kusaidia wengine kwa kutarajia zawadi

5. Katika hali zipi miongoni ya ifuatazo maneno ya mtu hutofautiana na vitendovyake?

   _____ Mtu mmoja huendelea kurudia kuwa sisi lazima tuwe wenye umoja lakini ana tabia ya kujenga mgogoro.

   _____ Mtu mmoja husifu thamani ya maisha ya ubikira lakini ana uhusiano wa ngono nje ya ndoa.

_____ Mtu mmoja anakunywa pombe mara moja moja ambapo anadai kufuata imani inayokataza unywaji pombe.

_____ Mtu mmoja anatetea usawa wa wanaume na wanawake, lakini, akiwa kama mwajiri yeye anawalipa wanawake ujira kidogokuliko wanaume kwa ajili ya kazi hiyo hiyo.

6. Inaruhusiwa kwa Mbahá'í kuungama kwa mtu mwingine? _____________________

7. Inampasa afanye nini badala ya kuungama? _____________________
_____________________

8. Maana ya "mbingu ya utukufu wa mbinguni" ni nini? _____________________
_____________________

9. Ni nini matokeo ya matendo mabaya duniani? _____________________
_____________________

10. Ni nini matokeo ya matendo mabaya kwa wale wanaoyatenda? _____________________
_____________________

## SEHEMU YA 3

Sasa soma na tafakari juu ya mateuzi yafuatayo kutoka Maandiko. Halafu jaribu kuyakariri.

**"Ukweli ndiyo msingi wa njema zote za binadamu."**[6]

1. Ni nini msingi wa njema zote za binadamu? _____________________
_____________________

**"Bila ukweli maendeleo na kufaulu, katika malimwengu yote ya Mungu, haviwezekani kwa roho yoyote."**[7]

2. Ni nini kisichowezekana bila ukweli? _____________________
_____________________

**"Rembesheni ndimi zetu, Enyi watu, kwa ukweli, na pambeni roho zenu kwa pambo la uaminifu."**[8]

3. Ni kwa kitu gani turembeshee ndimi zetu? _____________________
_____________________

4. Ni kwa kitu gani turembeshee roho zetu? ___________________________________

___________________________________________________________________

> **"Acha jicho lako liwe safi, mkono wako mwaminifu, ulimi wako wa ukweli, na moyo wako mwongofu."[9]**

5. Jicho letu linafaa liweje? _________________ Mkono wetu? ___________________

   Ulimi wetu? _______________________ Moyo wetu? _______________________

> **"Wale wanaoishi katika Hema Takatifu la Mungu, na wamewekwa imara kwenye viti vya utukufu wa milele, watakataa, hata kama wakiwa wanakufa kwa njaa, kunyoosha mikono yao, na kunyang'anya kinyume cha sheria mali ya jirani yao, japokuwa awe muovu na asiye thamani."[10]**

6. Ni nini Wabahá'í wanapaswa kukataa kufanya hata kama wanakufa kwa njaa?_____

___________________________________________________________________

___________________________________________________________________

## SEHEMU YA 4

Kama mlivyo kuwa mmeona katika Sehemu ya 2, baadhi ya mazoezi katika kitengo hiki yanahitaji majibu kamili. Katika hali kama hizo, kama kuna wasiwasi kuhusu jibu, mkufunzi wa kikundi chenu ataweza kukusaidia wewe na washiriki wenzako kufikia umoja wa wazo. Kwa mazoezi mengine, ni maongezi yenyewe ambayo yana thamani, na siyo jibu moja maalum linalotaajiwa. Katika mazoezi yafuatayo, zoezi la 3 ni la aina ya kwanza, wakati zoezi la 6 hudondokea kwenye aina ya pili.

1. Ukweli ndiyo msingi wa njema zote za binadamu.Orodhesha njema tano za binadamu. ___________________________________________________________

___________________________________________________________________

___________________________________________________________________

2. Je, tunaweza kujipatia njema hizi bila ukweli? _______________________________

3. Ni ipi kati ya kauli zifuatazo ni kweli?

   _____ Mtu anaweza kuwa mwenye haki, hata kama anasema uongo.

   _____ Mtu yule anayeiba ana mkono mwaminifu.

   _____ Mkono mwaminifu kamwe hauwezi kugusa kile kisicho chake.

   _____ Kusoma vitabu na magazeti yanayoeleza mambo ya ngono ni kinyume cha ushauri wa Bahá'u'lláh kuwa na jicho lililo safi.

______ Ukweli unamaanisha kutosema uongo.

______ Uaminifu ni pambo la roho.

______ Mtu asiye na ukweli anaweza kuendelea kiroho.

______ Ni sawa kusema uongo mara moja moja.

______ Kuiba kunakubaliwa mbele ya Mungu, ikiwamtu ana njaa.

______ Kuchukua kitu bila kibali cha mwenyewe, tukifikiri kwamba tutakirudisha baadaye, si kuiba.

______ Tukitenda kwa uaminifu na kuwa wenye haki na wakweli, moyo wetu ni mwongofu

______ Haiwezekani kuwa na biashara yenye mafanikio bila kudanganya kidogo.

4. Je, inawezekana kujidanganya mwenyewe? ______________________________

5. Ni nini tunachopoteza tunaposema uongo? ______________________________

6. Dunia ingekuwaje kama sote tungekuwa wenye ukweli na waaminifu? __________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

## SEHEMU YA 5

Soma nukuu zifuatazo na jaribu kujifunza bila kutamka. Kukariri nukuu kutoka kwenye Maandiko ni kitu kinachoridhisha sana, na inabidi mjitahidi sana kufanya hivyo. Walakini, wapo baadhi ya watu ambao hufikiri kukariri ni jambo lisilo wezekana kwa sababu tofauti. Ikiwa ninyi mnapata shida kukariri, inawabidi kujitahidi kusoma sana nukuu kiasi kwamba muweze kueleza kwa maneno yenu wenyewe mawazo ambayo ni karibu kabisa na Maandiko yenyewe.

**“Ulimi mwema ni sumaku ya mioyo ya watu. Ni mkate wa roho, unavisha maneno kwa maana.Ni chemchemi ya mwangaza wa hekima na akili.”**[11]

1. Ulimi mwema unaweza kuelezwaje? ______________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

2. Ni matokeo gani ambayo ulimi mwema huwa nayo kwa maneno? __________

______________________________________________________________

**"Enyi wapendwa wa Bwana! Katika kipindi hiki kitakatifu cha Maongozi ya Mungu, ugomvi na kushindana kwa vyovyote haviruhusiwi kamwe.Kila ngomvi hujinyima mwenyewe rehema za Mungu."[12]**

3. Kulingana na teuzi la hapo juu, ni kitu gani kisichoruhusiwa katika kipindi cha Maongozi ya Mungu? ______________________________________________

______________________________________________________________

4. Mgomvi hujifanyia nini mwenyewe? ___________________________________

______________________________________________________________

**"Hakuna chochote kinachoweza, katika siku hii, kutia madhara makuu zaidi kwenye Hoja hii kuliko mafarakano na kushindana, utengano na utepetevu, kati ya wapendwa wa Mungu."[13]**

5. Ni hali zipi zinaweza kutia madhara makubwa mno kwenye hoja ya Mungu? ______

______________________________________________________________

______________________________________________________________

**"Usiridhike na kuonesha urafiki wa maneno tu; acha moyo wako uwake kwa wema wa upendo kwa wale wote ambao waweza kupita njia yako."[14]**

6. Ni aina gani ya urafiki ambayo haipaswi kuturidhisha? ______________________

______________________________________________________________

7. Ni nini hupaswa kuwaka kwa wangavu katika moyo wetu? ___________________

______________________________________________________________

**"Wakati wazo la vita likija lipinge kwa wazo la nguvu zaidi la amani.Wazo la chuki lazima liangamizwe kwa wazo la uwezo zaidi la upendo."[15]**

8. Ni nini yapasa ilipinge wazo la vita? ___________________________________

______________________________________________________________

9. Ni nini yapasa iliangamize wazo la chuki? _______________________________

______________________________________________________________

## SEHEMU YA 6

Ukiwa na mateuzi ya hapo juu akilini, fanya mazoezi yafuatayo:

1. “Sumaku” ni neno lingine la magnetisi. Ni kwa njia gani ulimi mwema unaweza kutenda kama sumaku? ____________________________________________________

2. Ni zipi ya kauli zifuatazo hutoka kwenye ulimi mwema?

_____ “Usinisumbue!”

_____ “Kwa nini huelewi hili?”

_____ “Utajali kusubiri, tafadhali?”

_____ “Watoto wa kutisha jinsi gani!”

_____ “Shukrani, wewe u mwema sana.”

_____ “Sina muda wowote kwa ajili yako sasa. Nina kazi nyingi?”

3. Katika hali zifuatazo ni zipi ambazo zinaonesha mabishano na ugomvi?

_____ Watuwawili wanatoa maoni tofauti katikaushauriano.

_____ Watu wawili wanakasirikiana na wanabishana kati yao wakati wa ushauriano.

_____ Watu wawili wanaacha kuhudhuria mkutano ya ibada wa kila juma kwa sababu hawaongeleshani.

_____ Wajumbe wa timu inayoshirikiana katika mradi wanaendelea kulalamika. Kila mmoja anasema kuwa wengine hawafanyi sehemu yao ya kazi.

4. Katika hali zifuatazo ni zipi ambazo zinaonesha dalili za mafarakano?

_____ Marafiki wawili wanapishana njiani lakini wanapuuziana.

_____ Mtu mmoja anafika kwenye mkutano wa ibada, na kila mmoja anamsalimia kwa furaha.

_____ Ingawa ni wapole mmoja kwa mwingine, wajumbe wawili wa kikundi hawataki kushiriki katika mradi mmoja pamoja.

5. Amua kama matamko yafuatayo ni kweli:

_____ Mtu anapaswa aseme kwa uhalisi yale anayofikiria kwa wengine na haidhuru kama mioyo yao itachukizwa.

_____ Ni sawa kusema uongo ili kujiepusha na ugomvi.

_____ Ugomvi unaweza kushindwa kwa upendo na wema.

_____ Maneno yana matokeo zaidi yakisemwa kwa upendo.

_____ Ni sawa kupigana na mtu mwingine kama ni makosa yake.

_____ Mtu ana haki ya kuwa mkali kwa wengine akiwa mgonjwa au mwenye huzuni.

_____ Si jambo jema kuwacheka wengine wakoseapo.

_____ Wakati hisia kaliikiwepo kati ya marafiki, kila mmoja yafaa afanye jitihada maalum ya kumkaribia mwingine.

_____ Wakati hisia kali ikiwepo kati ya marafiki, kila mmoja yafaa asubiri mpaka mmoja afanye jitihada ya kumkaribia mwingine.

## SEHEMU YA 7

Soma mateuzi hapo chini na uyakariri:

**“. . . Usengenyaji huzima mwanga wa moyo, na hufisha uhai wa roho.”**[16]

**“Usinong’one dhambi za wengine iwapo wewe mwenyewe ni mtenda dhambi.”**[17]

**“Usiseme uovu, ili usiweze kuusikia ukisemwa kwako, na usiyakuze makosa ya wengine ili makosa yako mwenyewe yasije yakaonekana makubwa . . .”**[18]

**“Ewe Mwana wa Kuwa! Ungewezaje kuyasahau makosa yako mwenyewe na kujishughulisha na makosa ya wengine?”**[19]

1. Ni matokeo gani ambayo usengenyaji unao kwa yule anayesengenya? ___________

 ___________________________________________________________________

2. Ni kitu gani yatupasa kujihadhari nacho kabla hatujaanza kufikiria juu ya dhambi za watu wengine? _____________________________________________________

 ___________________________________________________________________

3. Ni kitu gani kitatokea kwetu tukiyakuza makosa ya wengine? __________________

 ___________________________________________________________________

4. Yatupasa tukumbuke kitu gani tunapofikiria makosa ya watu wengine? __________

 ___________________________________________________________________

## SEHEMU YA 8

Ukiwa na mateuzi ya hapo juu akilini, fanya mazoezi yafuatayo:

1. Ni kitu gani kinatokea kwa maendeleo ya roho ya mtu ambaye humulika makosa ya watu wengine? _____________________________________________________

2. Je, usengenyaji una matokeo gani kwa jumuiya? _____________________________

 ___________________________________________________________________

3. Utafanyaje wakati rafiki mmoja anaanza kuzungumza juu ya makosa ya mwingine?

______________________________________________________________

4. Amua kama kauli zifuatazo ni kweli:

_____ Tukizungumzia juu ya makosa halisi ya mtu, hatusengenyi.

_____ Tukizungumzia juu ya sifa nzuri za mtu, pamoja na makosa yake wakati ule ule hatusengenyi.

_____ Usengenyaji umekuwa mazoea katika jamii yetu nayatupasa kukuza maadili ya kuepukana nao.

_____ Msikilizaji akiahidi kutorudia yale tunayoyasema juuya mtu mwingine, hakuna madhara katika usengenyaji.

_____ Usengenyaji ni mmojawapo ya maadui wakubwa kabisa wa umoja.

_____ Tukijipatia mazoea ya kuzungumza juu ya watu wengine wakati wote, tu katika hatari ya kuanguka katika usengenyaji.

_____ Wakati uwezo wa watu mbalimbali unapojadiliwa katika mkutano wa Baraza la Kiroho la Mahali ili kuteua wajumbe wa kamati, huu ni usengenyaji.

_____ Wakati tusikiapo kusengenya, yatupasa tufikirie juu ya makosa yetu wenyewe.

_____ Tukijua kuwa mtu anafanya jambo ambalo linadhuru Imani, tunapaswa tulizungumzie na wajumbe wa jumuiya.

_____ Tukijua mtu yeyote anafanya jambo ambalo linadhuru Imani, tunapaswa tujulishe Baraza la Kiroho la Mahali.

_____ Si makosa kwa watu waliooana kuzungumza juu ya makosa ya wengine kwa sababu wanapaswa wasiwe na siri kati yao.

## SEHEMU YA 9

Kusudi la kitengo hiki, kama ilivyotajwa hapo mwanzoni ni kuwasaidia washiriki katika juhudi zao za kukuza na kuimarisha tabia ya kusoma vifungu kutoka Maandiko Matakatifu kila siku na kutafakari juu ya maana yao. Kusoma aya za Mungu kila asubuhi na jioni ni fundisho la Bahá'u'lláh linalopelekea kwenye ukuaji wetu wa kiroho. Kifungu kifuatacho kinatukumbusha kuhusu fadhila tunazopokea kwa kulikamilisha jukumu hili na unahamasishwa kuyakariri:

> **"Jizamisheni wenyewe katika bahari ya maneno Yangu, ili muweze kufungua siri zake na kugundua lulu zote za busara ambazo zimejificha katika vina vyake."[20]**

Baada ya kumaliza kitengo hiki, pengine sasa ungependa kupata kitabu cha maandiko ya Bahá'u'lláh na kukisoma kila siku. Maneno Yaliyofichwa ni chaguo la kwanza lililo nzuri.

## MAREJEO


1. Bahá'u'lláh, akitajwa na Shoghi Effendi, katika *Ujio wa Haki Takatifu* (Wilmette: Bahá'í Publishing Trust, 2006, 2018 printing), aya. 39, ku. 36–37.

2. *Mateuzi kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh* (Wilmette: Bahá'í Publishing Trust, 1983, 2017 printing), CXXXIX, aya. 8, uk. 345.

3. Bahá'u'lláh, *Maneno Yaliyofichwa* (Wilmette: Bahá'í Publishing Trust, 2003, 2012 printing), Kiarabu na. 31, uk. 11.

4. Kama hapo juu, Kiajemi na. 5, uk. 24.

5. Kama hapo juu, Kiajemi na. 69, uk. 46.

6. 'Abdu'l-Bahá, akitajwa na Shoghi Effendi, katika *Ujio wa Haki Takatifu*, aya. 40, uk. 39.

7. Kama hapo juu.

8. *Mateuzi kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXXXVI, aya. 6, uk. 336.

9. *Nyaraka za Bahá'u'lláh Zilizofunuliwa baada ya Kitáb-i-Aqdas* (Wilmette: Bahá'í Publishing Trust, 1988, 2005 printing), na. 9.5, uk. 138.

10. *Mateuzi kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXXXVII, aya. 3, uk. 338.

11. Kama hapo juu, CXXXII, aya. 5, uk. 327.

12. *Wosia na Agano wa 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Bahá'í Publishing Trust, 1944, 2013 printing), uk. 26.

13. *Mateuzi kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, V, aya. 5, uk. 8.

14. Kutoka hotuba iliyotolewa 16 na 17 October 1911, imechapishwa katika *Mazungumzo ya Paris: na'Abdu'l-Bahá katika 1911*(Wilmette: Bahá'í Publishing, 2006, 2016 printing), na. 1.7, uk. 6.

15. Kutoka hotuba iliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá 21 Oktoba 1911, kama hapo juu, na. 6.7, uk. 22.

16. *Mateuzi kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXXV, aya. 3, uk. 300.

17. *Maneno Yaliyofichwa*, Kiarabu na. 27, uk. 10.

18. Kama hapo juu, Kiajemi na. 44, uk. 37.

19. Kama hapo juu, Kiarabu na. 26, uk. 10.

20. *Mateuzi kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, LXX, aya. 2, uk. 154.



# Sala

## Kusudi

Kutafakari juu umuhimu wa sala na kuimarisha tabia ya kusali mara kwa mara

## SEHEMU YA 1

Kozi za Taasisi ya Ruhi zimekusudiwa kusaidia washiriki kutembea njia ya huduma. Tunatembea njia hii tukisukumwa na hisia ya kusudi lenye pande mbili—kukua kiroho na kiakili na kuchangia kwenye mmbadiliko wa jamii. Sura hizi mbili za kusudi letu haziwezi kutenganishwa kati yao. Bahá'u'lláh anatusihi katika kifungu kimoja:

> **"Msijishughulishe wenyewe katika masuala yenu wenyewe; yaache mawazo yenu yakaziwe juu ya kile ambacho kitarudisha mustakabali wa jamii ya wanadamu na kutakasa mioyo na roho za watu."[1]**

Katika fungu lingine, Yeye anaweka wazi kuwa:

> **". . . kusudi ambalo kwalo wanadamu, kutoka utupu kamili, wamekanyaga katika ufalme wa uwepo, ni kwamba wao waweze kufanya kazi kwa ajili ya uboreshaji wa ulimwengu na kuishi pamoja kwa umoja na upatano."[2]**

Kufuatana na hali yetu ya ndani, Yeye anatangaza:

> **"Moyo uliotakasika ni kama kioo; kisafishe kwa mng'aro wa upendo na kujitenga kutoka yote isipokuwa Mungu, ili jua la kweli liweze kung'aa ndani yake na alfajiri ya asubuhi ya milele"[3]**

Na 'Abdu'l-Bahá anatuambia:

> **"Mioyo yenu sharti iwe imetakasika na nia zenu zenye ukweli ili muweze kuwa wapokeaji wa majaaliwa matukufu."[4]**

1. Ni nini sharti uwe mkazo wa fikra na matakwa yetu? ___________________________

   ____________________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________________

2. Kwa kusudi gani tumeingia kutoka utupu kamili kuingia katika ufalme wa uwepo? _

   ____________________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________________

3. Ni kwa kitu gani tunapaswa kusafisha kioo cha moyo wetu? _____________________

   ____________________________________________________________________________

4. Ni baadhi ya hali zipi zinazovutia majaliwa matakatifu?________________________

   ____________________________________________________________________________

5. Yoyote miongoni mwa yafuatayo ni kweli?

   - Kwanza inakupasa ujitunzemwenyewe, na halafu ndiyo uwatunze wengine.

- Kama daima wewe unawasaidia wengine, hatimaye utashindwa kuona malengo yako mwenyewe.

- Wewe ndiye rafiki wa karibu zaidi.

- Jambo ambalo ni muhimu ni kutafutakile kinachokufurahisha.

- Fuata ndoto zako, na zitakufikisha kwenye furaha.

- Maadamu wewe humuumizi yeyote, haijalishi unacho kifanya.

- Ni sawa kuwa na sababu za kibinafsi, maadamu unafanya wema fulani.

## SEHEMU YA 2

Imani kuu kwa kusudi letu lenye pande mbili ni kwamba sote tumeumbwa bora. Bahá'u'lláh husema:

> **"Ewe Mwana wa Roho! Nilikuumba tajiri, kwa nini unajishusha mwenyewe kwenye umaskini? Nilikuumba Bora, kwa nini unajishusha mwenyewe? Kutoka katika kiini cha maarifa Mimi nilikupa uhai, kwa nini unatafuta elimu kutoka kwa mwingine kando Yangu? Kutoka katika udongo wa upendo Mimi nilikuumba, kwa jinsi gani unajishughulisha na mwingine? Geuzia macho yako kwako mwenyewe, ili uweze kuniona Mimi nikisimama ndani mwako mwenye nguvu, mwenye uwezo, na alijitoshelezaye."**[5]

Kwa kujaza nafasi wazi zilizopo hapo chini itakusaidia kutafakari juu ya kifungu hiki.

"Ewe Mwana wa Roho! Nilikuumba ________ , kwa nini unajishusha mwenyewe kwenye ____________ ? _____________ , kwa nini _______________ mwenyewe? Kutoka katika ________________________ cha ________ Mimi nilikupa uhai, kwa nini ______________________ kutoka kwa mwingine kando _________ ? Kutoka katika udongo ________________ Mimi ________________ , kwa jinsi gani ______________________ na ______________ ? Geuzia ________ yako __________ mwenyewe, ili uweze kuniona _________ nikisimama ndani mwako ____________ _________ , ________________ , na ______________________ ."

Kuwa wakweli kwa ubora wa roho zetu, lazima tugeukie Chanzo cha uwepo wetu na kutafuta mwangaza kutoka Kwake. Mojawapo ya njia za uhakika ni kupitia sala. Shoghi Effendi, Mlinzi wa Imani, anatuambia kuwa lengo lake kuu ni "maendeleo ya mtu na jamii, kupitia upatikanaji wa sifa njema za kiroho na uwezo. Ni roho ya mtu ambayo kwanza inahitaji kulishwa. Na chakula hiki cha kiroho kinaweza kutolewa na sala vizuri zaidi."[6]

## SEHEMU YA 3

Mungu ni Mjua yote, Mwenye Hekima yote. Yeye ametuumba na anajua kile kilichomo katika mioyo yetu na kile kinachotufaa zaidi. Yeye hahitaji sala zetu. Hivyo kwa nini tunasali?

‘Abdu’l-Bahá anasema:

> **“Katika sala ya juu kabisa, watu huomba tu kwa ajili ya upendo wa Mungu, si kwa sababu wanamuogopa Yeye au jehenam, au hutumaini kupata fadhila ua kuingia mbinguni. . . . Pale mtu ampendapo mwanadamu mwingine, hawezi kujizuia kutaja jina la mpenzi wake. Ni vigumu vilivyoje kuacha kutaja Jina la Mungu wakati mtu amekwishampenda Yeye. . . . Mtu wa kiroho hapati furaha kabisa katika chochote kile ila katika kumbukumbu ya Mungu.”**[7]

Na, kama jibu kwa swali moja, Yeye anaeleza:

> **“Ikiwa mtu mmoja anampenda mwingine, ni kawaida rafiki,siyo kawaida kuwa aseme hiyo? Ingawa yeye anajua kwamba rafiki anatambua upendo wake, kwani yeye hapendi kumwambia juu ya upendo wake? . . . Ni kweli kwamba Mungu anajua matakwa ya mioyo yote; lakini msukumo wa kuomba ni ule wa kawaida, unaobubujika kutoka upendo wa mtu kwa Mungu.”**[8]

1. Kamilisha sentensi zifuatazos:

   a. Katika _____________________ sala, tuna ________________ tu kwa ajili ya Mungu, siyo kwa sababu tuna muogopa Yeye au ______________ , au hutumaini kupata _____________________ au __________________ .

   b. Pale tuangukapo kwenye ________________ na binadamu mwingine, ni kwa ajili ____________ ni vigumu vilivyoje kuacha kutaja ___________________ la _____________ wetu. Ni vigumu _____________ kuacha ___________ Jina la __________ wakati mtu _________________________ Yeye.

   c. Mtu wa kiroho hapati ___________________ katika chochote ila katika _________________________ ya Mungu.

2. Kwa nini tuna sali? ____________________________________________________

   ____________________________________________________________________

3. Kifungu cha maneno “kumbukumbu ya Mungu” ina maana gani? _______________

   ____________________________________________________________________

4. Mtu anayempenda sana mwingine, anatamani sana kitu gani? __________________

   ____________________________________________________________________

5. Msukumo wa kusali unabubujika kutoka wapi? ______________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 4

Katika sala iliyofunuliwa na Bahá'u'lláh, tunasoma:

**"Ninakusihi Wewe . . . ifanye sala yangu moto ambao utateketeza tando ambazo zimenifungia nje ya Uzuri Wako, na mwanga ambao utaniongoza kwenye bahari ya Uwepo Wako."[9]**

Sisi twamuomba Mungu katika sala hiyohiyo:

**"Ifanye sala yangu, Ee Bwana Wangu, chemchemi ya maji yenye uzima ambayo kwayo niweze kuishi kadiri enzi Yako idumuvyo, na niweze kukutaja Wewe katika kila ulimwengu wa malimwengu Yako."[10]**

1. Ni katika mantiki gani sala inaweza kuwa kama moto? Inateketeza nini? _________

______________________________________________________________________

2. Taja baadhi ya tando zinazotufungia njenkutoka kwa Mungu: ___________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

3. Je sala inaweza kuwa kama mwanga? Inatuongoza kuelekea wapi? ______________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

4. Je sala inaweza kuwa kama chemchemi ya maji ya uhai? Inajalia nini juu ya roho zetu?

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 5

Soma na tafakari juu ya maneno yafuatayo ya 'Abdu'l-Bahá:

**"Hakuna kitu tamu zaidi katika ulimwengu wa uhai kuliko sala. Binadamu lazima aishi katika hali ya sala. Hali iliyobarikiwa zaidi ni hali ya sala na kuomba. Sala ni mazungumzo na Mungu. Pato kuu kabisa au hali iliyo tamu zaidi si nyngine ila mazungumzo na Mungu. Hufanyiza hali ya kiroho, hufanyiza**

**ufahamivu na maono ya mbinguni, hufanya mivuto mipya ya Ufalme na huamsha mwelekeo wa akili ya juu sana."[11]**

1. Hali gani ni tamu kabisa katika ulimwengu wa uwepo? ________________________

________________________________________________________________________

2. Kifungu cha maneno "hali ya sala" humaanisha nini? ________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

3. Taja baadhi ya mielekeo inayoletwa na sala: ________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

4. Pitia mateuzi ambayo mmekwishasoma katika sehemu hizi chache na andika sentensi tano juu ya asili ya sala.

   - Sala ni ________________________________________________
   - Sala ni ________________________________________________
   - Sala ni ________________________________________________
   - Sala ni ________________________________________________
   - Sala ni ________________________________________________

## SEHEMU YA 6

Soma maneno yafuatayo ya Bahá'u'lláh na yatafakari:

**"Imba, Ee mtumishi Wangu, aya za Mungu ambazo umezipokea, kama ziimbwavyo na wale ambao wamemkaribia Yeye, ili utamu wa wimbo wako mzuri uweze kuwasha moyo wako mwenyewe, na kuvutia mioyo ya watu wote. Yeyote asemaye, faraghani chumbani mwake, aya zilizofunuliwa na Mungu, malaika watawanyao wa Mwenyezi Mungu watatawanya mbali manukato ya maneno yatamkwayo na mdomo wake, na yataufanya moyo wa kila mtu mwadilifu kupuma.Ingawa, mara ya kwanza, atabakia bila kujua matokeo yake, lakini nguvu ya neema ijaliwayo kwake lazima papo hapo au baadaye iwe na mvuto katika roho yake.Hivyo ndivyo siri za Ufunuo wa Mungu zilivyoamriwa kwa nguvu ya Mapenzi ya Yeye Ambaye ndiye chanzo cha uwezo na hekima."[12]**

1. Neno "imba" humaanisha nini? ________________________________

________________________________________________________________________

2. Ni kwa jinsi gani tunapaswa kuziimba aya za Mungu? ________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

3. Neno “sema” humaanisha nini? __________________________________________
______________________________________________________________________

4. Neno “tawanya” humaanisha nini? ________________________________________
______________________________________________________________________

5. Ni matokeo gani utamu wa sauti zetu utakuwa nayo kwenye roho zetu wenyewe? __
______________________________________________________________________

6. Ni matokeo gani utamu wa sauti zetu unakuwa nayo kwenye mioyo ya wengine?___
______________________________________________________________________
______________________________________________________________________

## SEHEMU YA 7

Unaweza kukariri vifungu viwili kutoka sala iliyofunuliwa na Bahá’u’lláh:

**“Ee Mungu, Mungu wangu! Usiangalie matumaini yangu na matendo yangu, la afadhali zaidi uangalie mapenzi Yako ambayo yamezunguka mbingu na dunia.Kwa Jina Lako Kuu kabisa, Ewe Bwana wa mataifa yote! Nimetamani tu kile Wewe ulichotamani, na kupenda tu kile Wewe upendacho.”**[13]

**“Wewe u juu mno kwa sifa ya wale ambao wako karibu Nawe kupanda kwenye mbingu ya ukaribu Wako, au kwa ndege wa mioyo ya wale ambao wamejitoa kwako kufikia mlango wa lango Lako.Nashuhudia kwamba Wewe umetakasika kupita sifa zote na mtakatifu kupita majina yote. Hakuna Mungu mwingine ila Wewe, Aliyetukuka kuliko wote, Mtukufu-Kabisa.”**[14]

## SEHEMU YA 8

‘Abdu’l-Bahá husema:

**“Inambidi mtumishi kumuomba na kutafuta msaada kutoka kwa Mungu, na kumuomba na kusihi msaada Wake. Hilo ndilo linalostahili daraja la utumishi, na Bwana ataamuru chochote Apendacho, kufuatana na hekima Yake kamili.”**[15]

Na Yeye Anaeleza:

**“Roho ina mvuto; sala ina matokeo ya kiroho. Kwa hiyo, tunasali ‘Ee Mungu! Mponye mgonjwa huyu!’ Pengine Mungu atatujibu. Inajalisha nani anasali? Hujibu sala za watumishi Wake wote. Hujibu sala za mmea huu. Mmea husali iwezekanavyo, Ee Mungu! Niteremshie mvua! Mungu hujibu sala, na mmea hukua. Mungu atamjibu kila mmoja.”**[16]

Nikawaida kuwa katika sala yetu sisi tunamuomba Mungu atukamilishie mahitaji yetu.Hivyo tunaiombea afya yetu na afya ya wapendwa wetu, tunayaombea maendeleo ya kiroho na ya kimwili ya familia zetu, na tunaomba kwa ajili yamwongozo. Tunaomba tupate nguvu, imani, na uthibitisho katika njia ya huduma. Katika kumuomba Mungu, bila shaka tunapaswa kukumbuka kuwa malengo yetu maishani ni kuweka nia yetu sambamba na ile Yake. Kwa hiyo tunapaswa kuomba kuwa Amri Yake kifanyike na tuwe tayari kuikubali. Kama mtakariri maneno yafuatayo ‘Abdu’l-Bahá, yatatumika kama chanzo cha shangwe na uhakika wakati wote:

**“Ee ewe uliyegeuzia uso wako kuelekea kwa Mungu! Fumba macho yako kwa vitu vyote vingine, na uyafumbulie kwenye milki ya Mtukufu Kabisa. Omba chochote ukitakacho Kwake pekee; tafuta chochote ukitafutacho kutoka Kwake pekee. Kwa mtazamo mmoja Yeye hujalia taraji mia moja elfu, kwa mtupo wa jicho Yeye huponya magonjwa mia moja elfu yasiyotibika, kwa tazamo la mara moja Yeye huweka kitulizo kwa kila donda, kwa mwinamo wa kichwa Yeye huachilia mioyo kutoka kwenye pingu za huzuni. Hufanya kama afanyavyo, na je tuna kimbilio gani? Yeye hutimiza nia Yake, huamuru Alitakalo. Hivyo ni bora zaidi kwako kuinaminisha kichwa chako katika utii, na uweke tumaini lako katika Bwana Mwenye Rehema Kabisa.”**[17]

## SEHEMU YA 9

Kutoka kila kitu tulichosoma hadi sasa, ni wazi kuwa kumgeukia Mungu katika sala ni hitaji muhimu la maisha ya kiroho. Ni tamu vilivyoje kumuomba Mungu mara baada ya kuamka asubuhi na usiku kabla ya kulala. Muda tunaotumia kusali kila siku na idadi ya sala tuzisemazo zinategemea mahitaji yetu na kiu yetu ya kiroho. Katika kila tukio, tunaweza kuchagua kutoka sala nyingi zilizofunuliwa na Bahá’u’lláh, Báb, na ‘Abdu’l-Bahá. Hata hivyo, Bahá’u’lláh pia amefunua sala tatu za faradhi za kila siku. Shoghi Effendi anasema:

**“Sala za faradhi ni tatu kwa idadi.Ile fupi kabisa ina aya moja tu ambayo sharti isemwe mara moja tu katika muda wa saa ishirini na nne wakati wa adhuhuri.Sala ya kadiri lazima isemwe mara tatu kila siku, asubuhi, adhuhuri na wakati wa jioni.Ile sala ndefu ambayo ina maelezo mengi zaidi kati ya hizi sala tatu ni sharti isemwe mara moja tu katika muda wa saa ishirini na nne, na wakati wowote mtu ajisikiapo kuisema.**

**“Muumini yu huru kabisa kuchagua sala yoyote kati ya hizi tatu, lakini ana wajibu wa kusema yoyote kati ya sala hizi tatu, kulingana na maagizo yoyote maalum ambayo yameambatana nazo.”**[18]

Na huendelea:

> **“Hizi sala za faradhi za kila siku, pamoja nanyingine chache maalum, kama Sala ya Kuponya, Waraka wa Ahmad, zimejaliwa na Bahá’u’lláh nguvu maalum na maana, na hivyo zapaswa kukubaliwa kama zilivyo na kusemwa na waumini kwa imani isiyo na shaka na uthibiti, ili kwazo waweze kuingia katika mazungumzo ya karibu zaidi na Mungu, na kujifungamanisha wenyewe kabisa zaidi na sheria Zake na maagizo.”**[19]

Sala tatu za faradhi zilizofunuliwa na Bahá’u’lláh husemwa na mtu binafsi. Aina ya sala ya pamoja ambapo sala ya kila siku ya faradhi ina somwa katika kundi kufuatana na mila fulani haipo kwenye Imani ya Kibahá’í. Sala kwa Aliyefariki ndiyo sala pekee ya lazima inayosomwa kwa watu wengi kama ilivyoelezewa na sheria ya Kibahá’í. Inatakiwa kusemwa mbele ya umati na mmoja kati ya wale waliopo, wakati kundi lililobaki likiwa limesimama kwa utulivu.

1. Neno “faradhi” lina maanisha nini? ________________________________________
   ____________________________________________________________________

2. Ni sala ngapi za kila siku zilizofunuliwa Bahá’u’lláh? ________________________
   ____________________________________________________________________

3. Je tunatakiwa kusema sala zote tatu kila siku? ______________________________

4. Kama tukichagua Sala Ndefu ya Faradhi, ni mara ngapi tunapaswa kuisema kwa kila siku? ______________________________________________________________

5. Ni mara ngapi tunapaswa kusema, kama tukichagua Sala ya Kati ya Faradhi?______

6. Ni mara ngapi tunapaswa kusema, kama tutachagua Sala Fupi ya Faradhi? ________

7. Taja baadhi ya sala ambazo zina nguvu maalum: ____________________________
   ____________________________________________________________________
   ____________________________________________________________________

8. Kama hujawahi kufanya hivyo, kariri Sala Fupi ya Faradhi:

> **“Ninashuhudia Ee Mungu wangu, kwamba Wewe umeniumba mimi kukujua Wewe na kukuabudu Wewe. Nahakikisha, katika wakati huu, juu ya unyonge wangu na uwezo Wako, juu ya umaskini wangu na utajiri Wako.**
>
> **“Hakuna Mungu mwingine ila Wewe, Msaada mashakani Aliyepo Mwenyewe.”**[20]

9. Tunashuhudia nini katika sala hii? ________________________________________
   ____________________________________________________________________
   ____________________________________________________________________
   ____________________________________________________________________

## SEHEMU YA 10

Sisi tunapaswa kukumbuka kuwa kuongeza kwa baraka tunazopokea kwa kutii sheria ya sala ya Faradhi na chakula tunachopata kutokana na usemaji wa sala nyingine kama mtu binafsi, roho zetu zinainuliwa, pale tunaposikia sala zikisomwa katika mikusanyiko, mikubwa au midogo. Bahá'u'lláh hutuambia:

> **"Kusanyikeni pamoja kwa furaha na urafiki na someni aya zilizofunuliwa na Bwana mwenye huruma. Kwa kufanya hivyo milango ya ujuzi wa kweli itafunguka kwa uwepo wenu wa ndani, na halafu mtahisi roho zenu zimejaaliwa na uthabiti na mioyo yenu imejawa furaha angavu."[21]**

Sisi sote twapata furahakubwa kutokana na ujuzikwamba kila mahali ulimwenguni, mikusanyiko ya ibada ambamo marafiki na majirani hukutana pamoja kuongea na Mungu inaendelea kuongezeka kwa maelfu. Nyumba ya Haki ya Ulimwengu huandika:

> **"Mikutano ya ibada ni fursa ambayo roho yoyote inaweza kushiriki, ikivuta pumzi ya manukato ya mbinguni, ikijipatia utamu wa sala, ikitafakari juu ya Neno la Uumbaji, ikisafirishwa kwenye mbawa za roho, na ikizungumza na Mmoja Apendwaye kabisa. Hisia ya urafiki na kusudi la pamoja hufanyizwa, hasa katika mazungumzo ya hali ya juu ya kiroho ambayo kiasili hutokea katika nyakati hizona kupitia humo 'mji wa moyo wa binadamu' unaweza kufunguliwa."[22]**

Tunapohisi kuwa tunataka kusali, tunatulia kwa ukimya kwa muda kidogo kusafisha akili zetu kwa kuondoa mambo ya ulimwengu huu. Tunaposali tunakazia mawazo yetu kwa Mungu. Baada ya kusema sala, tunabaki kimya kidogo na hatuanzi kufanya shughuli yingine mara moja. Ndivyo hivyo tunavyo fanya tunaposikiliza sala zinazosomwa na wengine katika mkusanyiko. Katika matukio kama haya, sisi tunahifadhi mwelekeo wa kiibada na kufuata maneno kwa karibu, kana kwamba ni sisi wenyewe tunayoyasema.

1. Tunapaswa kukusanyika kwa roho gani tunapo sema aya za Mungu? ____________

   ____________________________________________________________

2. Ni yapi yatakuwa matokeo ya kukutana kwetu pamoja kwa ajili ya kusema aya za Mungu? ____________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

   ____________________________________________________________

3. Mikutano ya ibada ni fursa ambayo roho yoyote inaweza

   – _________ ,
   – ________________________________________ ,
   – ________________________________________ ,
   – ________________________________________ ,

– ____________________________________________________________ na
– ____________________________________________________________ .

4. Ni hisia gani zinazaliwa katika mkutano wa ibada? ____________________________

____________________________________________________________________

5. Ni zipi athari za maongezi ambayo yameboreshwa kiroho yanayotokea kwa kawaida katika mikutano wa ibada? ____________________________________________

____________________________________________________________________

6. Andika maneno machache kuhusu mwelekeo wenye heshima tunaotakiwa kuwa nao wakati wa kusali, ikiwa tuko peke yetu, ama katika mkusanyiko.

____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________
____________________________________________________________________

## SEHEMU YA 11

Kitengo cha kwanza cha kitabu hiki kililenga juu ya tabia za kusoma aya kutoka Maandiko kila siku na kufikiria juu ya maana yao. Hapa umetafakari juu ya maana ya sala kama matokeo yake tumeimarisha desturi ya kusali kila siku. Sehemu iliyotangulia imekuletea umakini juu ya umuhimu wa ibada ya jumuiya. Yote uliyojifunza hadi sasa yamekuandaa kufanya ukihitaji, kitendo cha kwanza juu ya njia ya huduma: kukaribisha mkutano wa ibada.

Kama hatua ya mwanzo, pengine unaweza kutaka kukariri sala kadhaa na kupata fursa ya kushiriki pamoja na marafiki wachache. Wakati huo huo, unaweza kuhakikisha kwamba unahudhuria angalau mkutano mmoja wa ibada wa jumuiya yako na unahesabika miongoni mwa wahimili wake wenye shauku. Hatimaye, basi, unaweza kuamua kukirimu mkutano wa ibada wewe mwenyewe, ukiwaalika marafiki zako, wajumbe wa familia na majirani kukusanyika kwa ajili ya ibada na undugu. Ni kawaida kwa washiriki wawili ama watatu wa kozi hii kuanzisha mkutano wa ibada kama huo pamoja.

Kama unavyoweza kufikiria, hakuna fomyula za jinsi mkutano wa ibada unavyopaswa kuandaliwa. Lakini ni wazi kuwa mkusanyiko huo ni wa marafiki ambamo sala zinatolewa, vifungu kutoka Maandiko vinasomwa, na maongezi yanayoinua yanafanyika—yote katika mandhari ambayo ni ya kiroho kwa uwazi. Je, unaweza kusema maneno machache kuhusu kila moja ya mawazo yafuatayo, katika muktadha wa kukaribisha mkutano wa ibada?

Kuwatumia mialiko yenye upendo: ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

Kuandaa mandhari yenye kukaribisha: ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

Kudumisha mandhari yenye heshima: ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

Kuendeleza undugu wenye furaha: ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

Kuhamasisha maongezi yenye kuinua ya kiroho: ______________________________

______________________________

______________________________

______________________________

## MAREJEO


1. *Mateuzi kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh* (Wilmette: Bahá'í Publishing Trust, 1983, 2017 printing), XLIII, aya. 4, uk. 105.

2. Bahá'u'lláh, katika *Uaminifu: Mkusanyo wa Nukuu kutoka Maandiko ya Kibahá'í*, zimekusanywa na Idara ya Utafiti Nyumba ya Haki ya Ulimwengu (London: Bahá'í Publishing Trust, 1987), na. 21, uk. 5.

3. *Wito wa Mpendwa Mtukufu: Iliyoteuliwa Maandiko ya Ghaib ya Bahá'u'lláh* (Haifa: Makao Makuu Bahá'í ya Ulimwengu, 2018), na. 2.43, uk. 31.

4. Kutoka hotuba iliyotolewa mnamo tarehe 5 Mei 1912, imechapishwa katika *Usambazaji wa Amani ya Ulimwengu: hotuba ziliyozolewa na 'Abdu'l-Bahá wakati wa ziara Yake huko Amerika na Canada katika mwaka 1912* (Wilmette: Bahá'í Publishing, 2012), uk. 127.

5. Bahá'u'lláh, *Maneno Yaliyofichwa* (Wilmette: Bahá'í Publishing Trust, 2003, 2012 printing), Kiarabu na. 13, ku. 6–7.

6. Kutoka barua ya tarehe 8 Desemba 1935 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi, imechapishwa katika *Sala na Maisha ya Ibada: Mkusanyo wa Nukuu kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh, Báb, na 'Abdu'l-Bahá na Barua za Shoghi Effendi na Nyumba ya Haki ya Ulimwengu, zimekusanywa na Idara ya Utafiti ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu* (Wilmette: Bahá'í Publishing, 2019), na. 71, uk. 31.

7. Maneno ya 'Abdu'l-Bahá, yamenukuliwa na J. E. Esslemont, *Bahá'u'lláh na Wakati Mpya: Utambulisho wa Imani ya Kibahá'í* (Wilmette: Bahá'í Publishing, 2006, 2017 printing), uk. 106.

8. Kama hapo juu.

9. Bahá'u'lláh, katika *Sala za Kibahá'í: Uteuzi wa Sala zilizofunuliwa na Bahá'u'lláh, Báb, na 'Abdu'l-Bahá* (Wilmette: Bahá'í Publishing Trust, 2002, 2017 printing), ku. 7–8.

10. Kama hapo juu, uk. 9.

11. Maneno ya 'Abdu'l-Bahá, yamenukuliwa katika *Nyota ya Magharibi*, tol. 8, na. 4 (17 May 1917), uk. 41.

12. *Mateuzi kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, CXXXVI, par. 2, uk. 334; pia katika *Sala za Kibahá'í*, uk. iii.

13. Bahá'u'lláh, katika *Sala za Kibahá'í*, ku. 8–9.

14. Kama hapo juu, uk. 12.

15. ‘Abdu’l-Bahá, katika *Sala na Maisha ya Ibada*, na. 24, uk. 7.

16. Kutoka hotuba iliyotolewa na ‘Abdu’l-Bahá tarehe 5 Agosti 1912, imechapishwa katika *Utangazaji wa Amani ya Ulimwengu*, uk. 345.

17. *Mateuzi kutoka Maandiko ‘Abdu’l-Bahá* (Wilmette: Bahá’í Publishing, 2010, 2015 printing), na. 22.1, ku. 75–76.

18. Kutoka barua ya tarehe 10 Januari 1936 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi, imechapishwa katika *Sala na Maisha ya Ibada*, na. 61, uk. 25.

19. Kutoka barua ya tarehe 10 Januari 1936 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi, ikinukuliwa katika *Sala za Kibahá’í*, uk. 301.

20. Bahá’u’lláh, katika *Sala za Kibahá’í*, uk. 4.

21. Bahá’u’lláh, katika *Sala na Maisha ya Ibada*, na. 68, uk. 29.

22. Kutoka ujumbe wa tarehe 29 Desemba 2015, imechapishwa katika *Muundo kwa ajili ya utendaji: Iliyoteuliwa Jumbe za Nyumba ya Haki ya Ulimwengu na zana za Nyongeza, 2006–2016* (West Palm Beach: Palabra Publications, 2017), na. 35.49, uk. 232.



# Uhai na Kifo

## Kusudi

Kuthamini kwamba maisha hayahusishi
mabadiliko tu na fursa za ulimwengu huu
lakini hutafuta maana yake ya kweli
katika ukuaji wa roho

## SEHEMU YA 1

Roho ya mtu imetukuzwa juu ya vitu na ulimwengu wa kimwili. Katika mojawapo ya hotuba Zake, 'Abdu'l-Bahá hueleza:

> **"Miili hii ya kimwili imeundwa na atomu; pale atomu zinapoanza kuachana kuoza huanza kutokea, alafu huja kile tunachokiita kifo. . . .**
>
> **"Kwa roho ni tofauti. Roho siyo muunganiko wa vitu, haijatengenezwa na atomu nyingi, ni kitu kisichogawanyika na kwa hiyo cha milele. Haimo kabisa katika utaratibu wa muumbo wa kimwili; roho haifi!"[1]**

1. "Kuundwa na" ina maanisha nini? ______________________________________________

   ______________________________________________________________________

2. Je, roho ya mwanadamu imejumuishwa na vipengele tofauti, kama ulivyo kimwili?

   ______________________________________________________________________

3. Je, roho yamwanadamu ni kitu cha kimwili? ______________________________

## SEHEMU YA 2

Barua moja iliyoandikwa kwa niaba ya Mlinzi inatamka kuwa "roho ya mwanadamu huja katika uwepo pale mimba inapotungwa".[2] Ikijibu swali kuhusu maana ya "mimba", Nyumba ya Haki ya Ulimwengu inatanabahi:

> **"Hakuna kilichopatikana kutoka maandiko ya Kibahá'í ambacho hususan kinaeleza wakati wa kibiolojia na asili ya tukio lililoelezwa kama 'mimba'. Matumizi ya msamiati katika muktadha wa kitabibu pia yanadhihirika kuwa siyo sahihi. Kwa uhakika, uelewa mmoja wa mimba ni kwamba unaenda sambamba na kuingia kwa mbegu ndani ya yai, tena nyingine ni baada ya kuingiza mbegu na upandikizaji, mwanzo wa ujauzito. Kwa hiyo pengine haitawezekana kujua ni lini ushirikiano wa roho pamoja na wa kimwili unapotokea, na maswali bado hayawezi kujibiwa kwa wazo la kiutu au uchunguzi kwa kuwa yanahusu siri za ulimwengu na asili ya roho yenyewe."[3]**

1. Roho ya mwanadamu inakuja lini katika uwepo? ____________________________

   ______________________________________________________________________

2. Je, msamiati "mimba" unaeleza tukio la kibiolojia kikamilifu? _________________

## SEHEMU YA 3

Muhusiano kati ya roho na mwili siyo ya kimwili; roho haingii wala kutoka mwilini na haichukui nafasi ya kiwiliwili. Ushirika wake pamoja na mwili unafanana na ule wa mwangaza na kioo ambamo unaakisika. Mwangaza unaoonekana katika kioo hauko ndani mwake. Vivyo hivyo, roho haimo ndani ya mwili. Kama 'Abdu'l-Bahá anavyoeleza,

> **"roho yenye mantiki, au roho ya mtu, haiishi kupitia mwili huu kiasili—hiyo ni kusema, haiingii ndani yake; kwa asili na kuingia ni tabia za miili, na roho yenye mantiki imetakasika juu ya hili. Kwa kuanza roho kamwe haingii ndani ya mwili, kwamba sharti iyahitaji makaazi, pindi inapouacha mwili. Hapana, mahusiano ya roho na mwili ni kama mahusiano ya taa hii na kioo. Kama kioo kimefutwa vizuri na kwa ukamilifu, mwangaza wa taa unaonekana ndani mwake, na kama kioo kimevunjika au kimefunikwa na vumbi, mwangaza utabaki umefichika."[4]**

1. Jaza nafasi wazi katika sentensi zilizopo hapa chini

   a. Roho yenye mantiki, au ____________________ , haishi kupitia mwili huu kiasili mwili kiasili — hiyo ni kusema, roho haina ________________________ .

   b. ____________________________ , au roho ya binadamu, haiingii mwilini; kasili na kuingia ni _____________________ , na roho yenye maniki ni _____________ .

   c. Roho kamwe ____________________________ kwa kuanza na, kwamba sharti iyahitaji pindi inapoucha, ______________________________________ .

   d. Uhusiano wa roho na mwili ni kama uhusiano wa __________________________ .

   e. Kama kioo kimefutwa vizuri na kwa ukamilifu, _________________________ huonekana ndani yake.

   f. Kama kioo kimevunjika au kufunikwa na vumbi ____________________________ .

2. Katika msingi wa kile ambacho tumekwisha jifunza mpaka sasa, amua kama yafuatayo ni kweli:

   ______ Roho siyo sehemu ya ulimwengu wa kimwili.
   ______ Roho imo ndani ya mwili.
   ______ Mwili ni mmiliki wa roho.
   ______ Roho haifi milele.
   ______ Mtu ana mwanzo wake pale roho inapojishirikisha yenyewe na kiinitete.
   ______ Maisha huanza pale mtu anapozaliwa katika ulimwengu huu.
   ______ Maisha ya kimwili ya mtu huendelea baada ya kifo.
   ______ Maisha hujumuisha mambo ambayo hututokea kila siku.

3. Tumia taswira ya mwanga na kioo kuelezea mahusiano kati ya roho na mwili: _____

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

## SEHEMU YA 4

Kuna uhusiano maalum sana kati ya roho na mwili ambavyo kwa pamoja hufanya binadamu.Uhusiano huu hudumu tu kwa muda mfupi wa maisha ya binadamu.Wakati uhusiano huu ukikoma, kila kimoja hurudi katika sehemu yake ya asili, —mwili kwenye ulimwengu wa vumbi, na roho kwenye malimwengu ya kiroho ya Mungu, ambako huendelea milele. ‘Abdu’l-Bahá hueleza:

> **“Roho ya mwanadamu ina mwanzo lakini haina mwisho: hudumu milele.”**[5]

Katika mojawapo ya hotuba Zake, Yeye anaweka bayana:

> **“Roho haihitaji mwili, lakini mwili unahitaji roho, la sivyo hauwezi kuishi. Roho inaweza kuishi bila mwili, lakini mwili bila roho hufa.”**[6]

Na Mlinzi anaeleza:

> **“Kuhusu roho ya mwanadamu: Kufuatana na Mafundisho ya Kibahá’í roho ya mtu inaanza pamoja na utungo wa kiinitete cha mwanadamu, na huendelea kukua na kupitia hatua zisizo na mwisho za uwepo baada ya kutengana na mwili. Maendeleo yake kwa hiyo hayana mwisho.”**[7]

1. Ukiwa na teuzi la hapo juu akilini, jibu maswali yafuatayo:

   a. Je, mwili unaihitaji roho? ______________________________

   b. Je, roho inauhitaji mwili? ______________________________

   ________________________________________________________

   c. Nini hutokea kwenye uhusiano kati ya mwili na roho tunapo kufa? __________

   ________________________________________________________

   d. Nini hutokea kwa roho baada ya kifo? ______________________

   ________________________________________________________

   e. Maendeleo ya roho hudumu kwa muda gani? __________________

   ________________________________________________________

f. Lini maisha hufikia kikomo? ________________________________________

________________________________________________________________

2. Amua ni yapi kati ya yafuatayo hukubaliana na kile ambacho tumekwisha jifunza katika sehemu hizi:

_____ Kifo ni adhabu.

_____ Uhusiano kati yamwili na roho hudumu urefu wa maisha ya uhai tu.

_____ Mwili una uwezo wa kuendelea milele.

_____ Roho itaendelea milele.

_____ Kifo ni mwisho wa uhai.

_____ Itakuwepo siku ya hukumu ambapo miili yetu itainuka tena.

_____ Wakati wa kifo, roho ina uhuru zaidi kuliko zamani.

_____ Maisha huishia na kifo.

_____ Tunapaswa kuogopa kifo .

_____ Chakula, mavazi, mapumziko ni lazima kwa ajili ya roho.

_____ Roho inachoka wakati mwili unapotumia nguvu zake.

_____ Roho haipati athari kutokana na maradhi au udhaifu wa mwili.

_____ Mwanadamu ataendelea kuwa na mahitaji ya kimwili baada ya kifo.

## SEHEMU YA 5

Sisi tumeona kuwa roho haichukui nafasi ya kimwili na haifanyi kazi kufuatana na sheria za kiasili, kama ifanyavyo miili. Roho inafanya ushawishi wake katika ulimwengu kupitia uwakala wa mwili, lakini hii siyo njia pekee ambayo inatumiwa na roho kutekeleza nguvu zake. Bahá'u'lláh anatamka:

> **"Kwa ukweli Ninasema, roho ya mtu imewekwa juu zaidi ya kuingia na kutoka. Inakuwa imesimama na wakati huohuo inapaa; inajongea lakinibado imesimama."[8]**

Na 'Abdu'l-Bahá anatuambia

> **"Juwa kuwa athari na utambuzi wa roho ya binadamu ni wa aina mbili; yaani, roho ya binadamu ina hali mbili za kufanya kazi na uelewa. Njia moja ni kupitia uwakala wa vyombo vya kimwili na viungo. Hivyo huona kwa macho; husikia kwa masikio; huongea kwa ulimi . . .**

> **"Njia nyingine ni athari ya roho na vitendo ni bila vyombo hivi vya kimwili na viungo."[9]**

1. Jaza katika nafasi wazi za sentensi zifuatazo:

   a. Roho ya mtu imewekwa juu zaidi ya ______________ na _________________ .

   b. Inakuwa __________________ na wakati huo huo _______________________ .

   c. Ina _______________________ , na wakati huo huo ina.

2. Eleza njia mbili ambazo kupitia humo roho inaleta athari zake ulimwenguni: ______

   ____________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________

3. Je, unaweza kutoa mifano ya ushawishi na utendaji wa roho bila vyombo vya kimwili?

   ____________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________

## SEHEMU YA 6

Sasa, kufuatana na majadiliano katika sehemu iliyotangulia, soma kifungu kifuatacho kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh:

> **"Juwa kuwa roho ya mwanadamu ipo juu zaidi, na huru kutoka madhaifu yote ya kimwili na kiakili. Ya kwamba mtu anayeumwa anaonesha dalili za udhaifu ni kutokana na vizuizi vinavyojiweka kati ya roho yake na mwili wake, kwa sababu roho yenyewe inabaki bila kuathirika kutoka maradhi yoyote ya kimwili. Fikiria mwangaza wa taa. Ingawa kitu kwa nje kinaweza kuingilia kati ya mnururiko wake, mwangaza wenyewe unaendelea kung'aa kwa nguvu zisizopungua, vivyo hivyo, kila maradhi yanayo shambulia mwili wa mwanadamu ni kizuizi kinachozuia roho kudhihirisha uwezo wake wa kiasili. Inapouacha mwili hata hivyo, itaonesha ukuu mkubwa sana na ushawishi mkubwa sana kiasi kwamba hakuna nguvu duniani inayoweza kulingana nayo. Kila roho iliyotakasika, kila roho nadhifu na roho takatifu itajaaliwa uwezo mkubwa sana, na itafurahia kwa shangwe kubwa sana."**[10]

1. Eleza katika maneno yako mwenyewe jinsi roho inavyobaki bila kuathiriwa na udhaifu wa mwili au akili, na kile kitakachowekwa wazi wakati wa kutengana kwake na mwili.

   ____________________________________________________________________

   ____________________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

2. Je, tutaendelea kudumisha nafsi yetu baada ya kifo cha miili yetu ya kibinadamu?

_______________________________________________________________

## SEHEMU YA 7

Bahá'u'lláh hutuambia:

**"Na sasa, kuhusu swali lako juu ya roho ya mtu na kuendelea kuishi kwake baada ya kifo.Jua wewe kwa ukweli kuwa roho, baada ya kutengana na mwili, itaendelea kwenda mbele mpaka ifikie ukaribu wa Mungu, katika kiwango na hali ambavyo mabadiliko ya nyakati na karne, hata mageuzi na nasibu za ulimwengu huu haviwezi kubadilisha.Itadumu kwa kadri ya Ufalme wa Mungu, enzi Yake, milki Yake, na uwezo Wake vitakavyodumu.Itadhihirisha ishara za Mungu na sifa zake, na itafunua wema wa upendo wa baraka Zake."**[11]

1. Roho itaendelea kwenda mbele kwa muda gani baada ya kutengana na mwili? _____

_______________________________________________________________

2. Roho itaendelea katika hali gani katika safari yake ya milele kuelekea mbele ya Mungu?_______________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

3. Roho itaonesha baadhi ya sifa na dalili zipi katika hali hiyo? ____________________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

4. Juu yamisingi ya yale tuliyosoma hadi sasa, amua kama yafuatayo ni kweli:

_____ Ufalme wa Mungu utadumu milele.

_____ Roho inauwezo wa kudhihirisha sifa za Mungu.

_____ Sala tuzisemazo kwa ajili ya waliyofariki haziathiri maendeleo ya roho zao.

_____ Kamwe roho haina ukomo wa kuishi.

## SEHEMU YA 8

Bahá'u'lláh hutangaza:

**"Fahamu kuwa kila sikio linalosikia, likihifadhiwa kwa utakaso na bila kunajisiwa, lazima wakati wote na kutoka kila upande litasikia sauti inayosema maneno matakatifu:'Kwa ukweli, sisi ni wa Mungu na Kwake tutarejea.' Siri za kifo cha kimwili cha mwanadamu hazijafichuliwa, na hadi sasa zinaendelea kubaki bila kusomwa. . . .**

**"Kifo kinampa kila muumini mwenye kujiamini kikombe cha uhai, kwa uhakika. Huleta shangwe, na ni mchukuzi wa furaha. Humpa zawadi ya uhai wa milele.**

**"Kuhusu wale ambao wameonja tunda la uwepo wa mwanadamu duniani, ambalo ni utambuzi wa Mungu mmoja wa kweli, utukuzwe utukufu Wake, maisha yao baada ya hapa yatakuwa ya namna ambayo haiwezi kuelezeka. Ujuzi huo anao Mungu peke Yake, Bwana wa malimwengu yote."[12]**

**"Ewe Mwana wa Mkuu kabisa! Mimi nimekifanya kifo mjumbe wa shangwe kwa ajili yako. Kwa nini unahuzunika? Nimefanya mwangaza umimine juu yenu uzuri wake. Kwa nini weweunajificha kutoka kwake?"[13]**

1. Ni kauli zipi kati ya zifuatazo ni kweli?

_____ Roho ya mwanadamu hutoka kwa Mungu na itarejea Kwake.

_____ Ujuzi wa uhai baada ya kifo anao Mungu.

_____ Kwa muumini anayejiamini, kifo ni uhai.

_____ Kifo ni mchukuzi wa furaha.

_____ Siri za kifo zinajulikana na wote.

_____ Tunapaswa kuthamini fadhila za maisha walakini tusiogope kifo, kwa sababu ni mjumbe wa furaha.

_____ Siyo muhimu kwetu kujua kuhusu uhai na kifo.

2. Sasa, wakati tunakumbuka kile tulichosoma katika sehemu hizi, andika aya fupi kuhusu uhai, kifo, mwili na roho.

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

_______________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

## SEHEMU YA 9

'Abdu'l-Bahá hueleza:

**"Katika mwanzo wa uhai wake, mwanadamu alikuwa katika ulimwengu wa tumbo la uzazi, ambamo alikuza uwezo stahiki wa kujiendeleza katika ulimwengu huu. Uwezo ambao unahitajika katika ulimwengu huu aliupata katika ulimwengu huo. Alihitaji macho katika ulimwengu huu; aliyapata katika ulimwengu wa tumbo la uzazi. Alihitaji masikio katika ulimwengu huu; aliyapata humo. Uwezo wote uliohitajika katika ulimwengu huu aliupata katika ulimwengu wa tumbo la uzazi. Katika ulimwengu ule alijiandaa kwa ajili ya ulimwengu huu, na alipoingia katika ulimwengu huu, aliona kuwa anamiliki vigezo vyote vya uwezo aliohitaji na alikuwa amepata viungo vyote vya nje na ndani vinavyohitajika kwa ajili ya maisha haya, katika ulimwengu ule. Kwa hiyo ni sawa kuwa katika ulimwengu huu pia lazima ajiandae kwa ajili ya ulimwengu mwingine mbele zaidi. Kile ambacho yeye anakihitaji katika ulimwengu wa Ufalme,lazima akipate na kukiandaa hapa. Kama vile alivyopata uwezo unaohitajika kwa ajili ya ulimwengu huu katika ulimwengu wa tumbo la uzazi, ndivyo hivyo, sharti apate kile ambacho atakihitaji katika ulimwengu wa Ufalme—yaani, uwezo wote wa mbinguni—katika ulimwengu huu."**[14]

1. Amua kama yafuatayo ni kweli ama hapana:

_____ Uwezo wote unaohitajika kwa ajili ya ulimwengu huu unapatikana katika ulimwengu wa tumbo la uzazi.

_____ Hakuna haja ya kujiandaa kwa ajili ya uhai katika ulimwengu ujao.

_____ Kile tunachohitaji katika ulimwengu wa Ufalme kitapatikana hukohuko.

_____ Kusudi la maisha haya ni kupata uwezo unaohitajika kwa ajili ya maisha katika ulimwengu ujao.

_____ Maisha ya kweli yanaanza pale mtu anapokufa na anapokwenda kwenye Ufalme mtukufu.

_____ Maisha ya kweli yanaanza katika ulimwengu huu na yanaendelea baada ya kifo cha kimwili.

2. Ni upi baadhi ya uwezo mwanadamu anaoupokea katika ulimwengu wa tumbo la uzazi? ______________________________________________

______________________________________________

3. Ni yapi baadhi ya majaliwa ambayo tunapaswa kuyapata hapa kwa ajili ya maisha baada ya kifo? ______________________________________________

______________________________________________

## SEHEMU YA 10

Bahá'u'lláh hutangaza:

**"Wajibu wote wa mtu katika siku hii ni kufikia ile sehemu ya furiko ya neema ambayo Mungu humwaga nje kwa ajili yake. Kwa hiyo, kusiwepo mtu yeyote atakayefikiria kuhusu ukubwa au udogo wa chombo chake.Sehemu ya wengine inaweza kuwa katika kiganja cha mkono, sehemu ya wengine inaweza kujaza kikombe, na wengine hata kipimo cha galoni."**[15]

1. Kufuatana na teuzi la hapo juu, jibu maswali yafuatayo:

   a. Ni upi wajibu wa kila mtu katika Siku hii? ______________________

   ______________________________________________

   b. Ni zipi baadhi ya baraka ulizozipokea kutoka kwa Mungu? ____________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   c. Neno "chombo" kinaongelea nini katika teuzi lililopo hapo juu? __________

   ______________________________________________

   d. Kwa nini hatupaswi kufikiria "ukubwa au udogo" wa uwezo ambao tumejaliwa?

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   e. Ni vipi baadhi ya vitu vinavyotukataza kupokea sehemu yetu ya neema ya Mungu? ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

   ______________________________________________

2. Amua katika yafuatayo yapi ni kweli?

_____ "Ukubwa au udogo" wa uwezo wetu humaanisha jinsi sisi tulivyo wajuzi.

_____ Kumtumikia Mungu, sisi tunahitaji kusahau madhaifu yetu na kuweka imani yetu yote Kwake.

_____ Kama katika ulimwengu huu sisi hatukuzi uwezo ambao Mungu ametujalia, roho zetu zitadhoofika pale tutakapofika katika ulimwengu ujao.

## SEHEMA YA 11

Bahá'u'lláh hueleza:

**"Umeniuliza Mimi kuhusu asili ya roho.Jua, kwa hakika, kwamba roho ni ishara ya Mungu, kito cha mbinguni ambacho uhalisi wake wale watu wenye elimu ya juu kabisa wameshindwa kuufahamu, na ambayo siri yake hakuna akili, hata iwe ipenyezayo jinsi gani, inaweza daima kutumaini kuivumbua.Ni ya kwanza miongoni mwa vitu vyote vilivyoumbwa kutangaza ubora wa Muumba wake, ya kwanza kutambua utukufu Wake, kushikilia kwenye ukweli Wake, na kumshujudia Yeye."**[16]

1. Jaza katka nafasi wazi katika sentensi zifuatazo:

a. Roho ni __________________________ ya Mungu.

b. Roho ni kito cha __________________ ambacho _____________ wale wenye elimu _____________ wameshindwa na ambayo ______________ hakuna akili, hata iwe ipenyezayo inaweza daima kutumaini _________________________ .

c. Roho ni _______________________________ kutangaza _________________ .

d. Roho ni ya kwanza ___________________________ utukufu wa Mungu.

e. Roho ni ya kwanza ku ____________________________ ukweli wa Mungu.

f. Roho ni ya kwanza ku ____________________________ katika uaminifu kwa Mungu.

2. Yapi miongoni ya yafuatayo ni kweli?

_____ "Kuvumbua" humaanisha kugundua.

_____ Miongoni mwa vitu vyote vilivyoumbwa, cha kwanza kumtambua Mungu ni ubongo wa mtu.

_____ "Ipenyezayo" humaanisha kali.

_____ Mtu mwenye ujuzi huelewa siri za roho.

_____ Wanafalsafa wakuu peke yao wanaweza kutangaza ubora Mungu.

_____ Hakuna ulazima wa kufikiria kuhusu roho kwa sababu hatuwezi kuielewa kamwe.

## SEHEMU YA 12

Bahá'u'lláh hutangaza:

**"Ninyi ni kama ndege anayepaa juu, kwa uwezo wote wa mabawa yake yenye nguvu, na kwa imani kamili na ya furaha, katika ukubwa wa mbingu, mipaka, akihimizwa kutosheleza njaa yake, hugeukia kwa shauku kwenye maji na udongo wa ardhi iliyo chini yake, na akisha nawsa katika wavu wa tamaa yake, hujikuta bila uwezo kurudia kuruka kwake kwenye milki alizotoka. Bila uwezo wa kukung'uta mzigo unaolemea mabawa yake yaliyochafuka, ndege huyo, hadi hapo mkaaji wa mbinguni, sasa hulazimika kutafuta makao katika mavumbi. Kwa sababu hii, Ee watumishi Wangu, msiyachafue mabawa yenu kwa udongo wa upotovu na tamaa za bure, na msiyaache yachafuliwe na vumbi wivu na chuki , ili msizuiliwe kuruka katika mbingu za elimu Yangu takatifu."**[17]

1. Kamilisha sentensi zilizopo hapa chini.

   a. Ndege ambaye Bahá'u'lláh anamsema katika teuzi hili ni ________________ .

   b. Ndege huyu ni mkaazi wa ______________________________________ .

   c. Kama mabawa yake yamechafuka ndege huyo analazimika kutafuta makaazi katika ____________ .

2. Sasa jibu maswali yafuatayo:

   a. "Mabawa" ya roho "yanachafuka" namna gani? __________________________

   ________________________________________________________________

   ________________________________________________________________

   b. Ni ipi baadhi ya mizigo inayofanana na "maji na udongo wa ardhi", unaoelemea juu ya mabawa ya roho? ______________________________________________

   ________________________________________________________________

   ________________________________________________________________

   c. Ni vipi baadhi ya vitu ambavyo vinaweza kutuzuia kupaa katika mbingu za ujuzi mtukufu? ________________________________________________________

   ________________________________________________________________

   ________________________________________________________________

d. Kwa nini roho inabadili makaazi yake ya mbinguni na kuyaacha kwa ajili ya makaazi ya vumbi la ulimwengu huu? ______________________________

______________________________________________________

______________________________________________________

3. Amua kama matamko yafuatayo ni kweli:

_____ Mwambatano na mambo ya kiulimwengu huzuia maendeleo yetu ya kiroho.

_____ Upotovu wetu na tamaa zenye utupu zinatuzuia kurudi kuruka katika mbingu za Ujuzi mtukufu.

_____ Husuda na chuki ni desturi za kiasili za mwanadamu na hazielemei roho.

_____ Tunaweza kujiondolea wenyewe mizigo ambayo inatuzuia kupaa katika ukubwa wa mbingu kwa kujikwamua kutoka vitu vya ulimwengu huu.

_____ Makaazi ya roho ni katika ulimwengu huu.

## SEHEMU YA 13

Bahá'u'lláh husema:

**"Alipomaliza kuumba ulimwengu na vyote viishivyo na kutembea humo, Yeye, kupitia utendaji wa moja kwa moja wa Mapenzi Yake, Mapenzi yasiyozuilika na ya enzi, Alichagua kumjalia mtu heshima ya kipekee na uwezo wa kumjua Yeye na kumpenda Yeye—uwezo mbao lazima ufikiriwe kuwa msukumo unaofanyiza na pia kuwa kusudi la msingi la muumbo wote. . . . Juu ya asili ya ndani kabisa ya kila kiumbe Yeye amemulika mwanga wa mojawapo wa majina Yake, na kuifanya mpokezi wa utukufu wa mojawapo wa sifa Zake. Juu ya asili ya mtu, walakin, Yeye amekazia mwanga wa majina na sifa Zake zote, na kuifanya kioo cha Nafsi Yake Mwenyewe. Pekee kati ya viumbe vyote mtu ameteuliwa kwa upendeleo mkuu mno kama huo, na Baraka inayodumu hivyo."**[18]

1. Jaza katika nafasi zilizopo hapa chini

a. Mungu alichagua kumjalia mwanadamu heshima na uwezo wa kipeke wa ______________________________ .

b. Juu ya uhalisi wa ____________ na ____________ Mungu alimulika mwanga wa __________ , nakuifanya mpokezi wa utukufu wa ________________ .

c. Juu ya uhalisi wa mwanadamu, Yeye amemulika mwanga wa ____________ , na kuifanya mpokezi wa ________________________ .

2. Sasa jibu maswali yafuatayo:

a. Je, unaweza kutaja baada ya sifa za Mungu? ______________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

b. Ni zipi baadhi ya sifa za Mungu mbazo roho ya kiutu inaweza kuakisi? ________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

c. Sifa hizi zinaweza kudhihirishwaje? ______________________________________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

d. Mwanadamu ameteuliwa kwa ajili ya upendeleo upi maalum? _______________

______________________________________________________________________

______________________________________________________________________

3. Ni yapi ni kweli miongoni ya yafuatayo?

_____ Mwanadamu siyo tofauti kutoka muumbo wote uliosalia.

_____ Uwezo wa kumjua Mungu na kumpenda Yeye ni msukumo anzilishi na kusudi la kimsingi lililopo kwenye mwanzo wa muumbo wote.

_____ Uhalisiwa kila kitu kilichoumbwa ni mpokeji wa sifa moja ya Mungu.

_____ Roho ya mwanadamu inaweza kuakisi sifa zote za Mungu.

## SEHEMU YA 14

Bahá'u'lláh hutuambia:

**"Nguvu hizi ambazo kwazo Nyota ya Mchana ya baraka za Mungu na Chanzo cha mwongozo wa mbinguni imejalia uhalisi wa mtu zimo, hata hivyo, kwa hali iliyofichika ndani mwake, hata kama vile mwali ulivyofichika ndani ya mshumaa na pia miali ya mwanga imo imefichika ndani ya taa.Uangavu wa nguvu hizi unaweza kutiwa giza na tamaa za dunia kama vile mwanga wa jua unavyoweza kufichwa chini ya vumbi na uchafu unaofunika kioo.Siyo mshumaa wala taa vyaweza kujiwasha kupitia nguvu zao zenyewe, wala daima haiwezekani kwa kioo kujiweka huru na uchafu wake.Ni wazi na dhahiri kwamba hadi pale moto uwashwapo taa haiwezi kamwe kuwaka, na kama uchafu haujaondolewa kutoka kwenye uso wa kioo hakiwezi kuonesha mfano wa jua wala kuakisi mwangaza na utukufu."**[19]

1. Nini maana ya neno “iliyofichaka”? ________________________________________

________________________________________________________________________

2. Ni upi baadhi ya uwezo ambao umejificha katika roho ya mtu? __________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

3. Taa ina uwezo gani? ____________________________________________________

4. Kioo kina uwezo gani? __________________________________________________

5. Unapaswa kufanyaje ili taa iweze kutoa mwangaza? ___________________________

________________________________________________________________________

6. Unapaswa kufanyaje ili kioo kiweze kuakisi mwangaza? ________________________

________________________________________________________________________

7. Je,taa na kioo vinaweza kuonesha uwezekano uliojificha zenyewe? ______________

8. Tunaweza kulinganishaje mifano hii miwili na hali yaroho ya mtu? ______________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

________________________________________________________________________

9. Nani anaweza kuifanya roho ya mtu ioneshe uwezo wake uliofichika? ____________

________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 15

Bahá’u’lláh hueleza:

**“Mlango wa elimu ya Yule Aliye Mkale daima umekuwa na utaendelea milele kuwa, umefungwa katika nyuso za watu. Hakuna ufahamu wa mtu yeyote daima utafikia ukumbi wake mtakatifu. Kama ishara ya rehema Yake, walakini, na kama uthibitisho wa wema Wake wa upendo, Yeye amedhihirisha kwa watu Nyota za Mchana za muongozo Wake mtakatifu, Alama za umoja Wake mtakatifu, na ameamuru kuwajua hawa Waliotakasika kama kumjua Yeye Mwenyewe.Yeyote awatambuaye Wao amemtambua Mungu.Yeyote asikilizaye na kujali mwito Wao, amesikiliza na kujali sauti ya Mungu, na yeyote ashuhudiaye ukweli wa Ufunuo Wao amemtambua Mungu.Yeyote asikilizaye na kujali mwito Wao, amesikiliza na kujali sauti ya Mungu, na yeyote ashuhudiaye ukweli wa Ufunuo Wao, ameshuhudia ukweli wa Mungu Mwenyewe. Yeyote**

**ageukiaye mbali kutoka kwao, amegeukia mbali kutoka kwa Mungu, na yeyote awakanaye Wao, amemkana Mungu. Kila mmoja Wao ni Njia ya Mungu ambayo huunganisha ulimwengu huu na milki za juu, na Kipimo cha Ukweli Wake kwa kila mmoja katika falme za duniani na mbinguni. Wao ni Wadhihirishaji wa Mungu kati ya watu, ushuhuda wa Ukweli Wake, na ishara za Utukufu Wake.”[20]**

1. Pamoja na teuzi lililopo hapo juu akilini, jibu maswali yafuatayo:

   a. Inawezekana kumjua Mungu moja kwa moja? ____________________________

   b. Tunawezaje basi, kumjua Mungu? ________________________________________

   ________________________________________________________________________

   c. Je, unaweza kutaja baadhi ya Nyota za Mchana za uongozi mtukufu? ________

   ________________________________________________________________________

   d. Wale waliowasikiliza Wadhihirishaji wa Mungu wamesikiliza sauti ya Nani?

   ________________________________________________________________________

   e. Tunamkengeukia nani tunapopuuzia wito wa Wadhihirishajiwa Mungu? ______

   ________________________________________________________________________

2. Kamilisha sentensi zifuatazo:

   a. Mlango wa ujuzi Yule Uwepo wa Kale daima umekuwa, na utaendelea kuwa ________________________________________________________________________ .

   b. Uelewa wa mtu yeyote hauwezi kamwe kufikia kwa ______________________ .

   c. Mungu aliwatuma Wadhihirishaji Wake kama alama Yake ya _____________ na kama ushahidi Wake ___________________________ .

   d. Ujuzi wa Wadhihirishaji wa Mungu ni sawa kabisa na ule wa _______________ _____________________________________ .

   e. Yeyote awatambuaye Wao ame ______________________________ .

   f. Yeyote asikilizaye wito Wao ame ______________________________________ .

   g. Kila mmoja Wao ni Njia ya Mungu ambayo _____________________________

   ________________________________________________________________________

   ________________________________________________________________________ .

3. Yapi miongoni mwa yafuatayo ni kweli?

   ______ Sisi tunaweza kukua kiroho kupitia juhudi zetu peke yetu.

   ______ Mungu ametupa akili, na inatosha kwa ajili ya maendeleo yetu.

_____ Sisi tutaendelea kiroho kwa kumtambua Mdhihirishaji wa Mungu na hatutahitaji kufanya juhudi yoyote nyingine.

_____ Sisi tutaweza kuendelea kiroho kwa kumtambua Mdhihirishaji wa Mungu na kufanya juhudiza kuishi kufuatana na mafundisho Yake.

_____ Sisi tunaweza kumjua Mungu moja kwa moja.

_____ Mwanadamu anaweza kuwa kama Mungu kabisa.

_____ Mungu ametukuka juu zaidi ya uelewa wamwanadamu.

_____ Pale tunaposikiliza maneno ya Mdhihirishaji wa Mungu, sisi tunasikiliza Sauti ya Mungu.

## SEHEMU YA 16

Bahá’u’lláh hutangaza:

**“Mitume na Wajumbe wa Mungu wameteleshwa kwa kusudi moja tu la kuiongoza jamii ya wanadamu katika Njia iliyoongoka ya Ukweli. Kusudi la msingi la ufunuo Wao limekuwa la kuwaelimisha watu wote, ili wao waweze, ifikapo saa ya kifo, kupaa, kwa utakaso kamili na utakatifu na kwa utengano kamili, kuelekea kiti cha enzi cha Yule aliye Juu Kabisa.”**[21]

Na katika kifungu kingine, Husema:

**“Mtu ni ile Talisimu iliyo kuu mno.Ukosefu wa elimu inayofaa, walakini, umemnyima kile ambacho kwa asili anacho.Kwa neno moja lililotoka kwenye kinywa cha Mungu aliumbwa; na kwa neno lingine zaidi aliongozwa kutambua Chanzo cha elimu yake; kwa neno lingine tena daraja lake na hatima yake vililindwa.Yule Aliyemkuu husema: Mfikirie mtu kama chimbo la madini lililojaa vito vya thamani kubwa.Elimu pekee, ndio inayoweza kulifanya lifichue hazina zake, na kuwezesha binadamu kufaidika kutoka kwake.Ikiwa mtu yeyote angetafakari yale ambayo Maandiko matakatifu yaliyoshushwa kutoka mbingu ya mapenzo matakatifu ya Mungu, yamefunua, angetambua upesi kwamba kusudi lao ni kwamba watu wote watafikiriwa kama roho moja, ili kwamba muhuri ulio na maneno haya ‘Ufalme utakuwa wa Mungu’ uweze kupigwa juu ya kila moyo, na mwanga wa baraka ya Mungu, wa neema, na rehema uweze kufunika binadamu wote.”**[22]

1. Mitume na Wajumbe wa Mungu wameteleshwa kwa kusudi lipi? _______________

_______________________________________________________________

_______________________________________________________________

2. Kuna kusudi gani kwenye msingi wa Ufunuo Wao? _________________________

_______________________________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

3. Neno “talisimu” lina maana gani? ______________________

______________________________________________

4. Ukosefu wa elimu sahihi una matokeo gani? ________________

______________________________________________

5. Elimu sahihi inaweza kusababisha nini? ___________________

______________________________________________

______________________________________________

6. Ni kipi chanzo cha elimu yetu? _________________________

7. Hatima yetu ni ipi? _______________________________

______________________________________________

8. Ni vipi baadhi ya vito ambavyo elimu huvifunua? ______________

______________________________________________

9. Tunatambua nini kwa utayari pale tunapo tafakari juu ya Maandiko Matakatifu? ___

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

______________________________________________

## SEHEMU YA 17

Bahá’u’lláh hueleza:

**“Umeniuliza, tena, kuhusu hali ya roho baada ya kutengana kwake na mwili. Jua wewe, kwa ukweli, kwamba ikiwa roho ya mtu imetembea katika njia za Mungu, kwa hakika itarudi na kukusanywa kwenye utukufu wa Mpendwa. Kwa haki ya Mungu! Itafikia daraja ambalo hakuna kalamu inayoweza kuifafanua, wala ulimi kuielezea. Roho ambayo imebakia aminifu katika hoja ya Mungu, na kusimama imara na thabiti katika Njia Yake, baada ya kupaa kwake, itakuwa na ile nguvu ambayo kwamba maulimwengu yote aliyoyaumba Mwenyezi Mungu yaweza kufaidika kupitia kwake.”[23]**

1. Kamilisha sentensi zifuatazo:

a. Ikiwa roho imetembea katika njia za Mungu, kwa hakika, ________________

________________________________________________________________

b. Itafikia daraja ambalo ____________________________________________

c. ______________ ambayo imebakia __________ katika _________________ ya ________________________ , na ime ______________________________ katika ___________ baada ____________ , itakuwa na ile ________________ kwamba malimwengu yote _________________ yanweza _______________ kupitia kwake.

## SEHEMA YA 18

Bahá'u'lláh hutuambia:

**"Imebarikiwa ile roho ambayo, wakati wa kuachana na mwili, imetakaswa kutokana na mawazo ya bure ya watu wa ulimwengu.Roho ya aina hiyo huishi na huenda kwa mujibu wa Mapenzi ya Muumba wake, na huingia katika paradiso iliyo juu kabisa.Wajakazi wa Mbinguni, wakaaji wa makao ya juu kabisa, wataizunguka, na Mitume wa Mungu na wateule Wake watatafuta urafiki wake. Na roho hiyo itazungumza kwa uhuru, na itawasimulia yale ambayo ililazimika kuvumilia katika njia ya Mungu, Bwana wa maulimwengu yote."[24]**

**"Yeye anapaswa amsamehe mwenye dhambi, na kamwe asidharau hali yake ya chini, kwa kuwa hakuna ajuaye vile mwisho wake mwenyewe utakavyo kuwa.Ni mara ngapi mtu mwenye dhambi amefikia, wakati wa kifo, kwenye kiini cha imani, na akigugumiza funda inayodumu milele, amepaa hadi Kundi la Umati wa juu! Na ni mara ngapi muumini mcha Mungu wakati wa kupaa kwa roho yake, amebadilika mno hata kuangukia kwenye moto wa chini kabisa!"[25]**

1. Roho yetu wakati wa kuachana na mwili, inatakiwa kuwa katika hali gani? _______

________________________________________________________________

2. Ni yapi baadhi ya mawazo matupu? ____________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

________________________________________________________________

3. Roho itaweza kutakaswanamna gani kutoka kwa mawazo matupu, kuishi na kujongea baada ya kifo? ____________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

4. Nani watakuwa wenzi wa roho kama hiyo? ______________________________

______________________________________________________________

5. Je, roho kama hiyo itaweza kuongea na Mitume wa Mungu na wateule Wake? ____

______________________________________________________________

6. Je, tunafahamu tangu mwanzo maisha yetu kiduniani yataisha jinsi gani na lini?

______________________________________________________________

7. Tunaweza kufanya nini sasa kupata maisha ya milele kama hatima yetu? _________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

## SEHEMU YA 19

‘Abdu’l-Bahá hueleza:

**“Kwa kuwa roho ya mwanadamu huishi milele baada ya kuvua mwili wake wa kidunia, kama vitu vyote vinavyoishi, bila shaka ina uwezo wa kuendelea, na hivyo mtu anaweza kusali kwa ajili ya roho iliyoondoka kuendelea, kusamehewa,au kufanywa chombo chenye kupokea fadhila, majaliwa, na neema. Ndiyo maana katika sala za Bahá’u’lláh, msamaha na usameheaji wa Mungu vinaombwa kwa ajili ya wale waliopaa kwenye ulimwengu ujao. Aidha, kama vile watu wanavyomhitaji Mungu katika ulimwengu huu, vivyo hivyo wao wanamhitaji katika ulimwengu ujao. Viumbe daima vinakuwa na mahitaji, na Mungu daima hana mahitaji kabisa, kama ni katika ulimwengu huu au katika ulimwengu ujao.”**[26]

1. Kwa nini sharti tusali kwa ajili ya roho ya aliyefariki?

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

______________________________________________________________

## SEHEMU YA 20

'Abdu'l-Bahá hueleza:

**"Pale roho ya mtu inapopaa kutoka lundo hili la vumbi la mpito na huinuka kwenda katika ulimwengu wa Mungu, basi tando zitaondoka, na kweli zitaonekana katika mwangaza, na vitu vyote visivyojulikana mwanzoni, vitawekwa wazi, na kweli zilizofichwa zitaeleweka.**

**"Fikiria jinsi kiumbe, katika ulimwengu wa tumbo la uzazi, alikuwa kiziwi masikioni na kipofu machoni, na bubu wa ulimi; jinsi yeye alivyokuwa hana utambuzi wowote. Lakini pindi, alipotoka katika ule ulimwengu wenye giza, yeye aliingia katika ulimwengu huu wenye mwangaza, hapo jicho lake liliona, sikio lake likasikia, ulimi wake uliongea. Kwa namna hiyo hiyo, pindi atakapoharakia mbali kutoka mahali hapa pa mauti, kuelekea Ufalme wa Mungu, basi hapo yeye atazaliwa katika roho; ndipo jicho la utambuzi wake litafunguka, sikio la roho yake litasikia, na kweli zote ambazo yeye alikuwa hazitambui kabla zitadhihirika kwa kawaida na kwa uwazi."**[27]

1. Jaza nafasi wazi hapo chini

   a. Pale roho ya mtu inapoacha ulimwengu huu, hapo

   - tando ____________________ ,
   - na kweli _________________________ ,
   - na vitu vyote vilivyokuwa havijulikani mwanzoni ______________________ ,
   - na kweli zilizofichika _________________________________ .

   b. Katika ulimwengu wa __________________ , sisi tulikuwa _______________ wa masikio, ________________ wa jicho, na ______________________________ wa ulimi.

   c. Tulipozaliwa katika ulimwengu huu, hapo jicho letu _____________ , sikio letu _____________________ , na ulmi wetu ______________________________ .

   d. Kwa namna hiyo hiyo, pindi atakapoharakia katika Ufalme wa Mungu, tutakuwa ________________________ katika _______________________________ .

   e. Hapo ndipo jicho letu la ________________ lita ______________ , sikio letu la ____________ lita ______________ , na yale yote ___________ tulikuwa hatuyajui mwanzoni yatawekwa ____________________ na ___________________ .

2. Amua kama matamko yafuatayo ni kweli:

_____ Tunapokuwa katika ulimwengu wa tumbo la uzazi, tujunua kuhusu ulimwengu huu.

_____ Hali yetu baada ya kifo ni ukweli uliofichwa kutoka kwetu katika maisha haya.

_____ Peo mpya kabisa, zitafunguka mbele yetu baada ya kifo.

_____ Tunapo kufa, sisi tunarudi kwenye ulimwengu huu kuzaliwa tena.

## SEHEMU YA 21

Bahá'u'lláh hueleza:

**"Na sasa kuhusu swali lako kama roho ya mtu inaendelea kutambuana moja kwa nyingine baada ya kutenganakwake na mwili. Fahamu kuwa roho za watu wa Bahá, ambao wameingia na wamesitawishwa ndani ya Bendera ya Safina, watashirikiana na kuongea kwa karibu mmoja na mwingine, na watashirikiana kwa karibu sana katika maisha yao, matumaini yao, malengo yao na jitihada za kujaribu kuwa kama roho moja. Wao kwa uhakika ni wale ambao wanataarifa kamili, wana uoni makini, na ambao wamepewa uelewa. Hivyo ndivyo ilivyoamriwa na Yule Ambaye ni Mjua Yote, Mwenye Hekima Yote.**

**"Watu wa Bahá, ambao ni wakazi wa Safina ya Mungu, kila mmoja wao anatambua vizuri daraja na hali ya mwenzake, na wameunganika katika mafundo ya ukaribu na undugu. Hali kama hiyo, hata hivyo, inategemea juu ya imani yao na vitendo vyao. Wao ni wa daraja moja na ngazi moja na wanatambua kabisa uwezo wa kila mmoja, tabia, mafanikio, na wanachostahili. Wale ambao ni wa daraja la chini, hata hivyo, hawawezi kuelewa kikamilifu ngazi, au kukadiria wanachostahili, ya wale ambao wako kwenye daraja la juu yao. Kila mmoja atapokea sehemu yake kutoka Bwana wako. Amebarikiwa yulemtu ambaye hugeuzia sura yake kwa Mungu, na anatembea kwa uthabiti katika upendo Wake, hadi roho yake itakapo ruka katika safari yake kwa Mungu, Bwana Mtawala wa wote, Mwenye uwezo wote, Msamehevu daima, Mwenye Rehema kabisa."[28]**

1. Katika ulimwengu ujao, je, sisi tutatambua watu ambao tumewafahamu katika ulimwengu? ______________________________

2. Ushirikiano huo kati ya roho utakuwa wa ukaribu kiasi gani katika ulimwengu ujao?

______________________________

3. Tofauti na upekee miongoni mwa roho unategemea nini katika ulimwengu unaokuja?

______________________________

______________________________

4. Kuna mtu yeyote atakaye nyimwa neema ya Mungu? ____________________________
_____________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 22

Bahá'u'lláh hutusihi:

**"Enyi watumishi Wangu! Msihuzunike kama, katika siku hizi na katika dunia hii ya kimwili, mambo yaliyo kinyume cha matakwa yenu yameamriwa na kudhihirishwa na Mungu, kwa kuwa siku zenye furaha nyingi, za nderemo ya mbinguni, bila shaka zimewekwa akiba kwa ajili yenu. Malimwengu, matakatifu na yenye utukufu wa kiroho, yatafunuliwa machoni mwenu. Mmekusudiwa na Yeye, katika ulimwengu huu na ule ujao, kujipatia sehemu ya manufaa yao, kushiriki katika furaha zao, na kujipatia sehemu ya rehema yao yenye msaada.Bila shaka mtafika kwa kila moja wao."**[29]

1. Amua yapi miongoni mwa yafuatayo ni kweli:

   ______ Sisi tunapaswa kujaa huzuni kama mambo hayaendi tunavyotaka kuwa.

   ______ Kila kitu, kama ni kizuri ama kibaya, kimeamriwa na Mungu.

   ______ Siku za shangwe kuu zinatusubiri sisi sote.

   ______ Sisi tuna uhakika wa kuona malimwengu ambayo ni matakatifu na matukufu kiroho.

   ______ Ni hatima yetu kushiriki katika manufaa ya malimwengu ambayo ni matakatifu na tukufu kiroho, pote pawili katika maisha haya na katika maisha ya baadaye.

2. Kwa nini hatupaswi kujaza huzuni pale ambapo mambo hayaendi kufuatana na matakwa yetu? ____________________________________________
_____________________________________________________________________________
_____________________________________________________________________________
_____________________________________________________________________________

3. Bahá'u'lláh anatuahidi nini katika kifungu hiki? ______________________________
_____________________________________________________________________________
_____________________________________________________________________________
_____________________________________________________________________________

## SEHEMU YA 23

Katika kitengo hiki, umetafakari juu ya maana ya maisha ya mwanadamu. Umejifunza mengi kuhusu asili ya roho, kusudi la maisha katika ulimwengu huu, ya lazima kwa ajili ya kukuza sifa za kiroho, na ahadi tuliyopewa ya uhai wa milele, uliotukuka na uliojazwa na shangwe. Katika kitengo cha pili cha kitabu hiki, sisi tuliongea juu ya kusudi lenye pande mbili—la kufuata ukuaji wetubinafsi wa kiroho na wa kiakili na la kuchangia kwa ubadilikaji wa jamii. Hapa ipo fursa ya kurudi kwenye wazo hilo na kufikiri juu ya maana inayowiana na sura zote mbili za kusudi hili, kufuatana na umaizi ambao umeupata juu ya maendeleo ya roho. Tafakari zako zinaweza kupata faida kutokana na majadiliano juu ya mada zilizopo hapa chini katika kikundi chako.

1. *Kukuza sifa za kiroho*
2. *Kutii sheria za Mungu*
3. *Kuchangia kwenye ustawi wa jamii ya wanadamu*
4. *Kuendelea kwenye njia ya huduma*

## MAREJEO


1. Kutoka hotuba iliyotolewa mnamo tarehe 10 Novemba 1911, imechapishwa katika *Mazungumzo ya Paris: na 'Abdu'l-Bahá katika 1911* (Wilmette: Bahá'í Publishing, 2006, 2016 printing), na. 29.12–13, uk. 109.

2. Kutoka barua ya tarehe 1 April 1946 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi, imechapishwa in *Miangaza ya Mwongozo: Bahá'í Reference File* (New Delhi: Bahá'í Publishing Trust, 1988, 2010 printing), na. 1820, uk. 537.

3. Kutoka barua ya tarehe 28 Julia 2016 iliyoandikwa kwa niaba ya Nyumba ya Haki ya Ulimwengu.

4. 'Abdu'l-Bahá, katika *Baadhi ya Maswali Yaliyojibiwa* (Wilmette: Bahá'í Publishing, 2014, 2016 printing), na. 66.3, ku. 352–53.

5. Kama hapo juu, na. 38.5, uk. 220.

6. Kutokahotuba iliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá tarehe 9 Novemba 1911, imechapishwa katika *Mazungumzo ya Paris*, na. 28.16, uk. 104.

7. Kutoka baruaya tarehe 31 Decemba 1937 iliyoandikwa kwa niaba ya Shoghi Effendi, imechapishwa katika *Miangaza ya Mwongozo*, na. 680, uk. 204.

8. *Mateuzi kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh* (Wilmette: Bahá'í Publishing Trust, 1983, 2017 printing), LXXXII, aya. 8, uk. 183.

9. 'Abdu'l-Bahá, katika *Baadhi ya Maswali Yaliyojibiwa*, na. 61.1–2, uk. 334.

10. *Mateuzi kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, LXXX, aya. 2, uk. 174.

11. Kama hapo juu, LXXXI, aya. 1, uk. 176.

12. Kama hapo juu, CLXV, aya. 1–3, ku. 391–92.

13. Bahá'u'lláh, *Maneno Yaliyofichwa* (Wilmette: Bahá'í Publishing Trust, 2003, 2012 printing), Kiarabu na. 32, uk. 11.

14. Kutoka hotuba iliyotolewa mnamo tarehe 6 Julia 1912, imechapishwa katika *Promulgation wa Universal Peace: Mazungumzo yaliyotolewa na 'Abdu'l-Bahá wakati wa Safari Zake kitengo hiki Anatamka na Canad katika 1912* (Wilmette: Bahá'í Publishing, 2012), ku. 315–16. (authorized translation)

15. *Mateuzi kutoka Maandiko ya Bahá'u'lláh*, V, aya. 4, uk. 8.

16. Kama hapo juu, LXXXII, aya. 1, ku. 179–80.

17. Kama hapo juu, CLIII, aya. 6, ku. 370–71.

18. Kama hapo juu, XXVII, aya. 2, ku. 72–73.

19. Kama hapo juu, XXVII, aya. 3, uk. 73.

20. Kama hapo juu, XXI, aya. 1, ku. 54–55.

21. Kama hapo juu, LXXXI, aya. 1, uk. 177.

22. Kama hapo juu, CXXII, aya. 1, ku. 293–94.

23. Kama hapo juu, LXXXII, aya. 7, uk. 182.

24. Kama hapo juu, LXXXI, aya. 1, ku. 176–77.

25. Kama hapo juu, CXXV, aya. 3, ku. 300–1.

26. ‘Abdu’l-Bahá, katika *Baadhi ya Maswali*, na. 62.3, ku. 340–41.

27. *Mateuzi kutoka Maandiko ‘Abdu’l-Bahá* (Wilmette: Bahá’í Publishing, 2010, 2015 printing), na. 149.3–4, ku. 246–47.

28. *Mateuzi kutoka Maandiko ya Bahá’u’lláh*, LXXXVI, aya. 1–2, ku. 192–93.

29. Kama hapo juu, CLIII, aya. 9, uk. 373.